



SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO

YA AMALI

MHE. LELA MUHAMED MUSSA (MBM)

**KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA
2024/2025**

Mei, 2024



Mhe. Lela Muhamed Mussa
Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
Zanzibar



Mhe. Ali Abdulgulam Hussein
Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
Zanzibar



Mr. Khamis Abdulla Said
Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali
Zanzibar



Mr. Khalid Masoud Wazir
Naibu Katibu Mkuu Utawala
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali
Zanzibar



Dkt. Mwanakhams Adam Ameir
Naibu Katibu Mkuu Taaluma
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali
Zanzibar

YALIYOMO

UTANGULIZI.....	1
MIRADI YA SEKTA YA ELIMU	5
UTEKELEZAJI WA KAZI ZA WIZARA KWA MWAKA 2023/2024.....	6
MUUNDO WA PROGRAMU.....	6
UTEKELEZAJI WA MPANGO WA WIZARA KWA MWAKA 2023/2024..	6
PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI	8
PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI.....	11
PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU.....	13
Programu ndogo ya Mafunzo ya Ualimu	14
Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti	15
Huduma ya Sayansi na Teknolojia.....	18
Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu.....	21
Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu.....	23
PROGRAMU YA NNE: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI..	25
Programu ndogo ya Mafunzo ya Amali	25
Programu ndogo ya Elimu Mbadala na Watu Wazima.....	28
PROGRAMU YA TANO: UBORA WA ELIMU	29
Huduma ya Mitaala na Vifaa vya Kufundishia	30
Huduma ya Upimaji na Tathmini ya Elimu.....	31
Huduma ya Ukaguzi wa Elimu	33
Huduma za Maktaba.....	35
Huduma ya Urajisi wa Elimu	37
Programu ndogo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu ..	38
Programu ndogo ya Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha.....	41

Programu ndogo ya Michezo na Utamaduni katika Skuli.....	43
PROGRAMU YA SITA: UTAWALA NA UONGOZI	45
Programu ndogo ya Uongozi Kijumla	45
Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti	47
Programu ndogo ya Uratibu shughuli za elimu Pemba	50
MAPATO.....	51
MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2024/2025 KATIKA MFUMO WA PROGRAMU.	51
Vipaumbele vya Wizara	51
MAELEZO YA PROGRAMU ZA ELIMU	54
PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI	55
PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI.....	57
PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU.....	58
Programu ndogo ya Mafunzo ya Ualimu	59
Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti	60
Huduma ya Elimu ya Sayansi na Teknolojia	61
Huduma ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu	62
Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu	64
PROGRAMU YA NNE: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI... 65	
Programu ndogo ya Mafunzo ya Amali	65
Programu ndogo ya Elimu Mbadala na Watu Wazima.....	66
PROGRAMU YA TANO: UBORA WA ELIMU	67
Huduma ya Mitaala na Vifaa vya Kufundishia	67
Huduma ya Upimaji na Tathmini ya Elimu.....	68
Huduma ya Ukaguzi wa Elimu	69
Huduma za Maktaba.....	69

Huduma ya Urajisi wa Elimu	71
Programu ndogo ya Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha.....	72
Programu ndogo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) .	73
Programu ndogo ya Michezo na Utamaduni katika Skuli.....	74
PROGRAMU YA SITA: UTAWALA NA UONGOZI	75
Programu ndogo ya Uongozi kiujumla	75
Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti	76
Programu ndogo ya kuratibu shughuli za Elimu Pemba.....	77
MAKADIRIO YA MAPATO	77
JUMLA YA GHARAMA ZA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI ..	78
SHUKURANI	79
VIAMBATISHO	80

**HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI
KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA
KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

UTANGULIZI

- Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu liingie katika Kamati ili niweze kutoa maelezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya Fedha ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2024/2025.
- Mheshimiwa Spika**, Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutujaalia uhai, uzima na afya njema tukaweza kukutana tena katika kikao hiki cha kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Aidha, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukamilisha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na tukaweza kusherehekea Sikukuu ya Eid-el-Fitr kwa salama na amani. Namuomba Mwenyezi Mungu atuzidishie kheri na baraka zake na aniwezeshe kuwasilisha hotuba hii kwa ufasaha mkubwa na awajaalie wasaa wajumbe wote wa baraza hili kuichangia vizuri na hatimae waweze kuipitisha kwa kauli moja.
- Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa kuendelea kuipa kipaumbele sekta ya Elimu iliyotupelekea sote kushuhudia mabadiliko makubwa ya

elimu ndani ya kipindi kifupi. Maamuzi haya ya Serikali yametuwezesha kutekeleza maazimio mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa kwa kiwango kikubwa tukaweza kufikia shabaha zilizowekwa zikiwemo za Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambazo kwa upande wa elimu tayari tumevuka shabaha kwa maeneo mengi. Aidha, Nichukuwe Fursa hii pia kumshukuru Mama Maryam Mwinyi, Mke wa Rais wa Zanzibar kwa mashirikiano na ukaribu anaotupa katika kuimarisha elimu Zanzibar.

4. **Mheshimiwa Spika,** Jitihada hizo za Serikali zina mchango mkubwa katika kuhakikisha upatikanaji wa fursa sawa ya elimu bora kwa wote sambamba na kuzalisha wataalamu wa fani mbalimbali ambao watalisaidia Taifa kwa kuliletea maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa na hatimaye kufikia malengo ya Taifa ya Dira 2050 ya kuifikisha Nchi yetu katika Uchumi wa kati na wa Juu. Namuomba Mwenyezi Mungu amzidishie afya njema, hekma, busara na maarifa zaidi Rais wetu Dk. Hussein Ali mwinyi, ili aendelee kutuongoza vizuri. Pia napenda kutoa pongezi zetu na shukurani za dhati kwa Makamo wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, kwa utendaji wao mzuri na kumpa mashirikiano ya karibu Mheshimiwa Rais.
5. **Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati kabisa nimshukuru na nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuimarisha

umoja wa Watanzania, amani na mshikamano ulioimarisha mashirikiano baina ya sehemu zote mbili za Muungano. Jitihada hizo zimesaidia sana kufanya kazi kwa kujiamini na kutujengea uwezo uliopelekea kutatua changamoto zetu nyingi zikiwemo udhamini wa wanafunzi wa elimu ya juu.

6. **Mheshimiwa Spika**, Pia nichukue fursa hii kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Mwenyekiti wa Baraza kwa kulingoza Baraza hili na kusimamia mijadala na hoja za Wajumbe katika kuchangia mipango na mikakati ya Serikali yenye kuchochea maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla. Namuomba Mwenyezi Mungu akuzidishieni busara, hekima, umahiri na uadilifu katika kutekeleza majukumu yenu. Aidha, nichukuwe fursa hii kumshukuru Katibu wa Baraza la Wawakilishi.
7. **Mheshimiwa Spika**, Niwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Ustawi wa Jamii wakiongozwa na Mwenyekiti wao shupavu Mheshimiwa Sabiha Filfil Thani kwa kuwa karibu sana nasi na kutupa mashirikiano na maelekezo ambayo matokeo yake yamesaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha sekta ya elimu nchini. Aidha, niwashukuru Wenyeviti na wajumbe wote wa Kamati zako mbali mbali. Pia niwashukuru sana wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa umakini wao na michango yao wanayoitoa kwa maendeleo ya nchi yetu.
8. **Mheshimiwa Spika**, Niwashukuru kwa dhati kabisa watendaji wote wa “Presidential Delivery Beureu” (PDB) Chini ya Mtendaji Mkuu wao Prof. Mohammed Hafidh

Khalfan, kwa mashirikiano wanayoendelea kutupatia katika maeneo mbalimbali yaliyosaidia utekelezaji wa Miradi ya Mikakati hasa ujenzi wa skuli. PDB pia walitusaidia kwa kiasi kikubwa katika kuratibu na kusimamia uwekezaji binafsi kwenye sekta ya elimu mfano wawekezaji wa kampuni ya ROK kutoka Uturuki waliojenga Skuli kubwa ya Kisasa eneo la Fuoni, na pia kushirikiana na Tony Blaire Institute katika kuwajengea uwezo watendaji wa WEMA kupitia mfumo wa Priority Project Results Agreement (PPRA).

9. **Mheshimiwa Spika,** Nichukuwe fursa hii pia kumshukuru na kumpongeza Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Mheshimiwa Ali Abdulghulam Hussein kwa kunipa mashirikiano makubwa katika kutekeleza majukumu ya Wizara hii. Pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wakiwemo Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu Utawala, Naibu Katibu Mkuu Taaluma, Afisa Mdhamini wa Elimu, Wakurugenzi, Wakuu wa vitengo, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi mbali mbali za Elimu, Maafisa wa ngazi mbalimbali wa Wizara, bila kusahau walimu na Kamati zetu za skuli kwa mashirikiano yao makubwa katika kuleta maendeleo ya elimu nchini. Aidha, shukurani ziwafikie wazazi, wanafunzi na wadau wote wa elimu wa ndani na nje ya nchi kwa ushiriki na michango yao katika kusaidia harakati za utoaji na upatikanaji wa huduma ya elimu iliyo bora kwa wote. Mwenyezi Mungu awazidishie moyo wa imani na uzalendo kwa nchi yetu.

10. **Mheshimiwa Spika**, Mwisho nawashukuru sana watendaji wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Tume ya Mipango, Ofisi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mkaguzi Mkuu wa Ndani, ZAECA na Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar na Taasisi nyengine kwa ushirikiano wao ambao umechangia katika kuimarisha huduma za elimu katika mwaka 2023/2024. Ni matumaini yetu kuwa ushirikiano huo utaimarika zaidi katika kuimarisha upatikanaji wa huduma za elimu bora katika Taifa letu.
11. **Mheshimiwa Spika**, Utekelezaji wa mpango wa elimu kwa mwaka wa fedha 2023/2024 umetokana na mchango mkubwa na mashirikiano yaliyojengeka kwa muda mrefu kati ya Serikali, Wananchi na Wahisani wa ndani na nje katika kuchangia utekelezaji wa miradi mbalimbali sambamba na kufikia malengo ya kitaifa.
12. **Mheshimiwa Spika**, kabla ya kuelezea matarajio ya bajeti ya mwaka 2024/2025, nitawasilisha utekelezaji wa mpango wa elimu kwa Mwaka wa fedha wa 2023/2024.

MIRADI YA SEKTA YA ELIMU

13. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ilitekeleza kazi zake kupitia miradi mikuu mitano kama ifuatayo:-
 1. Uimarishaji wa Miundombinu ya Elimu
 2. Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi na Msingi
 3. Uimarishaji wa Elimu ya Sekondari
 4. Uimarishaji wa Elimu ya Juu
 5. Uimarishaji wa Elimu ya Amali

UTEKELEZAJI WA KAZI ZA WIZARA KWA MWAKA 2023/2024

- 14. Mheshimiwa Spika,** sasa naomba kuwasilisha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024 kupitia programu sita za elimu.

MUUNDO WA PROGRAMU

- 15. Mheshimiwa Spika,** programu kuu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ni sita kama zifuatazo:-

Programu ya 1: Elimu ya Maandalizi na Msingi

Programu ya 2: Elimu ya Sekondari

Programu ya 3: Elimu ya Juu

Programu ya 4: Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali

Programu ya 5: Ubora wa Elimu

Programu ya 6: Uongozi na Utawala

UTEKELEZAJI WA MPANGO WA WIZARA KWA MWAKA 2023/2024

- 16. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mpango wa elimu kwa mwaka wa fedha 2023/2024 umezingatia Programu kuu sita zinazoakisi malengo ya maendeleo ya elimu ya Kitaifa na Kimataifa ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050, vipaumbele vya sekta, Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Maagizo ya Mheshimiwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

- 17. Mheshimiwa Spika,** Programu hizo zote zilitekelezwa kwa mashirikiano makubwa kati ya Serikali, Jamii na Washirika wa Maendeleo wa ndani na nje ya Zanzibar. Programu hizi zilitengewa jumla ya **TSh. 457,299,603,000**. Kati ya fedha hizo, **TSh. 276,228,600,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida, zikiwemo **TSh. 221,464,600,000** za malipo ya mishahara na **TSh. 54,764,000,000** za matumizi mengineyo. Aidha, **TSh. 181,071,003,000** kwa kazi za maendeleo zikiwemo **TSh. 98,970,736,000** kutoka SMZ na **TSh. 82,100,267,000** kutoka kwa Wahisani wa maendeleo.
- 18. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **TSh. 340,226,661,543** sawa na asilimia **74** ya makadirio zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **TSh. 195,978,750,827** sawa na asilimia 88.6 zimetumika kulipia mishahara ya wafanyakazi na **TSh. 28,378,212,823** sawa na asilimia 51.8 zimetumika kwa matumizi mengineyo. Kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya **TSh. 115,869,697,893** zilipatikana. Kati ya fedha hizo, **TSh.99,803,098,430** sawa na asilimia **101** ni kutoka SMZ na **TSh.16,066,599,463** sawa na asilimia **20** ni kutoka kwa wahisani ambapo shughuli nyingi za Miradi ya Wahisani zinategemea kukamilika kwa taratibu za Manunuzi zinazoendana na miongozo yao.
- 19. Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji halisi kwa kila Programu ni kama ifuatavyo:-

PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI

- 20. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inahusisha uimarishaji na utoaji wa elimu ya maandalizi na msingi kwa wanafunzi wenye umri kati ya miaka minne hadi kumi na mbili.
- 21. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ilitengewa jumla ya **TSh. 131,918,709,000** Kati ya fedha hizo **TSh. 95,431,337,000** ni kwa ajili ya kazi za kawaida zikiwemo **TSh. 84,783,251,000** za Mishahara, **TSh. 10,648,086,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 36,487,372,000** kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Aprili, 2024, jumla ya **TSh.107,866,938,443** sawa na asilimia **82** zilipatikana. Fedha hizo zilitumika kutekeleza shughuli zifuatazo:-
- i). Ukarabati wa skuli 18 za Maandalizi na Msingi umekamilika katika skuli za Ndagoni, Ole, Maziwang'ombe, Jojo, Shumbaviamboni, Pujini, Pondeani, Machomane, Kipange, Ngezi, Mauwani, Chumbuni, Chutama, Maungani, Uzini Msingi, Jang'ombe Maandalizi, Kizimbani Msingi na Mahonda. Aidha, ukarabati unaendelea katika skuli za Kidongochekundu na Magogoni.
 - ii). Ujenzi wa skuli 2 za ghorofa umekamilika pamoja na kupatiwa samani katika maeneo ya Donge msingi na Fuoni kwa Unguja. Aidha, ujenzi unaendelea katika skuli 6 za Unguja na Pemba.
 - iii). Wizara imekamilisha ujenzi wa vyoo 146 katika skuli 11 za maandalizi na msingi kwa Unguja na Pemba.

- iv). Jumla ya wanafunzi 63,732 wa ngazi ya elimu ya Maandalizi na 20,807 wa ngazi ya elimu Msingi katika Skuli 42 za Serikali wanafaidika na huduma ya chakula kupitia mradi wa lishe. Aidha, Wizara inaendelea kutoa ruzuku kwa wanafunzi 63,732 wa ngazi ya elimu ya Maandalizi na 324,460 wa ngazi ya elimu ya Msingi katika skuli za Serikali.
- v). Skuli mbili za wanafunzi wenye mahitaji maalum zenye dakhalia zilizopo katika maeneo ya Jendele Unguja na Pujini Pemba zimeanza masomo rasmi ambapo jumla ya wanafunzi 228 (150 Unguja na 78 Pemba) wameandikishwa na wanafunzi 117 wenye ulemavu wanaishi dakhalia.
- vi). Jumla ya walimu 439 wamepangiwa kazi katika skuli za Maandalizi na Msingi Unguja na Pemba. Walimu 366 kati ya hao (127 Unguja na 239 Pemba) ni kati ya walimu waliojitolea. Aidha, walimu 73 (Unguja 53 na Pemba 20) wamepangiwa kazi kwa ajili ya kufundisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Matokeo ya muda Mfupi

- i) Jumla ya wanafunzi 103,475 sawa na asilimia 84.3 wameandikishwa katika ngazi ya elimu ya maandalizi. Kati yao wanaume ni 51,957 sawa na asilimia 84.2 na wanawake ni 51,518 sawa na asilimia 84.5. Jadweli namba 13(a) linatoa ufafanuzi zaidi.

- ii) Jumla ya wanafunzi 391,398 sawa na asilimia 104.4 wameandikishwa katika ngazi ya elimu ya msingi. Kati yao wanaume ni 197,301 sawa na asilimia 105.1 na wanawake ni 194,097 sawa na asilimia 103.7. Jadweli namba 14 linatoa ufafanuzi zaidi.
- iii) Jumla ya wanafunzi 58,128 wapya wameandikishwa kuanza darasa la kwanza kwa mwaka 2024. Kati yao 29,287 ni wanaume na 28,841 ni wanawake. Kati ya wanafunzi walioandikishwa darasa la kwanza, Wanafunzi 51,584 sawa na asilimia 88.7 wamepitia elimu ya maandalizi. Jadweli namba 15(C) linatoa ufafanuzi zaidi.
- iv) Uwiano wa walimu kwa wanafunzi ngazi ya elimu ya maandalizi umepungua kutoka 32 mwaka 2023 hadi kufikia 29 mwaka 2024.
- v) Uwiano wa wanafunzi kwa darasa ngazi ya elimu maandalizi umepungua kutoka 53 mwaka 2023 hadi kufikia 52 mwaka 2024.
- vi) Uwiano wa walimu kwa wanafunzi ngazi ya elimu msingi umepungua kutoka 45 mwaka 2023 hadi kufikia 42 mwaka 2024.
- vii) Uwiano wa wanafunzi kwa darasa ngazi ya elimu msingi umepungua kutoka 62 mwaka 2023 hadi kufikia 60 mwaka 2024.

PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI.

22. Mheshimiwa Spika, Programu hii inalenga kutoa na kuimarisha elimu ya Sekondari. Jumla ya **TSh. 190,707,359,000** zimepangwa kutumika, kati ya fedha hizo **TSh. 107,410,933,000** ni kwa ajili ya kazi za kawaida zikiwemo **TSh. 93,779,483,000** kwa ajili ya mishahara na **TSh. 13,631,450,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 83,296,426,000** kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Mwezi Aprili 2024, jumla ya **TSh. 156,454,334,893** sawa na asilimia **82** zilipatikana. Utekelezaji kwa programu hii ni kama ifuatavyo:-

- i. Ujenzi wa skuli 5 za ghorofa umekamilika pamoja na kupatiwa samani katika maeneo ya Mtopepo na Tumejuja kwa Unguja na Kiwani, Maziwang'ombe na Utaani kwa Pemba. Aidha, Wizara inaendelea na ujenzi wa skuli 13 kwa Unguja na Pemba.
- ii. Wizara imekamilisha ujenzi wa vyoo 46 katika skuli 2 za Sekondari za Fidel Castro na Jongowe.
- iii. Ukarabati wa Skuli za Sekondari umefanyika katika skuli mbalimbali zikiwemo skuli ya Muyuni Sekondari, Faraja Sekondari, Kengeja-Dakhalia Sekondari, Mikunguni, Ukumbi wa Skuli ya Sekondari Fidel Castro, Dakhalia ya wanafunzi wa Kiume Lumumba, Chaani Sekondari, TC Kiembesamaki na Maktaba.
- iv. Wizara imenunua vifaa vya maabara na kemikali kwa ajili ya Mitihani ya Taifa ya Kidato cha Nne na cha Sita

na kusambazwa katika skuli 193 za Sekondari zenye madarasa ya kidato cha nne na skuli 18 zenye kidato cha sita kwa Unguja na Pemba. Aidha, vifaa mbalimbali vya ufundi vimesambazwa katika skuli za Sekondari za ufundi Unguja na Pemba.

- v. Jumla ya TSh. 1,124,750,000 zimelipwa kwa ajili ya gharama za watahiniwa 22,495 wa kidato cha nne na TSh. 115,650,000 zimelipwa kwa gharama za deni la mithani kwa watahiniwa 2,313 wa kidato cha sita waliofanya mitihani mwezi wa Mei mwaka 2023. Aidha, jumla ya Tsh. 359,398,000 zimetumika kununulia vifaa vya maabara kwa ajili ya mtihani wa Kidato cha Nne mwaka 2023.
- vi. Wizara inaendelea kutoa ruzuku za uendeshaji wa skuli 217 za Sekondari Unguja na Pemba ambapo jumla TSh. 378,279,696 zimetumika. Aidha, TSh. 73,200,000 zimetolewa kwa ajili ya ruzuku za uendeshaji wa vituo 22 vya ubunifu wa kisayansi (School Hubs) Unguja na Pemba.
- vii. Jumla ya wanafunzi 3,378 wa Unguja na Pemba wanaoishi dakhalia wamehudumiwa na TSh. 1,265,980,000 zimetumika kwa ajili ya gharama za huduma ya chakula.

Matokeo ya muda mfupi

- i. Jumla ya wanafunzi 116,764 (wanaume 53,319 na wanawake 63,445) sawa na asilimia 63.8

wameandikishwa katika ngazi ya Elimu ya Sekondari ya awali (Kidato 1 – 4). Jadweli namba 16(a) linatoa ufafanuzi zaidi.

- ii. Asilimia ya uandikishaji imeongezeka kutoka asilimia 58 mwaka 2023 hadi kufikia asilimia 63.8 mwaka 2024.
- iii. Wastani wa Uwiano wa wanafunzi kwa darasa ngazi ya Sekondari imefikia 41 mwaka 2024 kulinganisha na shabaha ya wanafunzi 45 kwa darasa. Hata hivyo, bado mtindo wa Shifti mbili unaendelea kwa asilimia 14 ya skuli za Sekondari.
- iv. Uwiano wa wanafunzi kwa mwalimu ngazi ya elimu ya Sekondari umefikia wanafunzi 20 kwa mwalimu mwaka 2024.

PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU

23. Mheshimiwa Spika, Madhumuni ya programu ya Elimu ya Juu ni kutoa elimu itakayomuwezesha muhitimu kujiajiri au kuajiriwa. Programu hii ina programu ndogo moja ambayo ni mafunzo ya ualimu na maeneo manne ya huduma, ikiwemo Huduma ya Ushauri na Utafiti; Huduma ya Sayansi na Teknolojia; Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu na Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu. Programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya **TSh. 58,724,112,000**. Kati ya fedha hizo, **TSh. 8,929,800,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida zikiwemo **TSh. 22,526,312,000** kwa ajili ya malipo ya mishahara na **TSh. 27,268,000,000** za matumizi mengineyo.

Hadi kufikia Aprili 2024, Jumla ya **TSh. 42,356,546,499** sawa na asilimia **72** zimepatikana. Utekelezaji wa programu hii ni kama ifuatavyo:-

Programu ndogo ya Mafunzo ya Ualimu

24. Mheshimiwa Spika, Madhumuni makubwa ya Programu hii ni kuwawezesha walimu kuwa wabunifu, wataalamu na wenye uwezo wa kuongoza ili kukuza ubora wa elimu. Programu hii ndogo inatekelezwa na Idara ya Mafunzo ya Ualimu. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 programu hii imepangiwa kutumia jumla ya **TSh. 1,232,612,000**. Kati ya fedha hizo, **TSh. 390,000,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 842,612,000** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2024, Jumla ya **TSh. 868,722,729** sawa na asilimia **70** zimepatikana. Utekelezaji halisi wa programu hii ni kama hivi ifuatavyo:-

- i. Wizara imekamilisha rasimu ya muongozo wa kuendesha mafunzo kazini kwa skuli (School Base Inservice Training- SBIT) ili walimu waweze kujengeana uwezo katika skuli husika. Aidha, Idara ya Mafunzo ya Ualimu inaendelea na kazi ya uandishi wa rasimu ya muongozo wa uendeshaji wa vituo vya walimu ili kuweza kutoa huduma kwa ufanisi zaidi.
- ii. Wizara kupitia Idara ya Mafunzo ya Ualimu imeandaa mfumo maalum wa kielektroniki wa kukusanya taarifa mbalimbali za walimu wanaopatiwa mafunzo kazini kwa lengo la kuweza kutambua utaalamu na ujuzi waliopata katika kukuza elimu nchini.

- iii. Wizara imefanya ufuatiliaji kwa walimu tarajali 828 katika skuli mbalimbali kwa lengo la kuona ufundishaji kwa njia ya vitendo baada ya kumaliza mafunzo ya darasani. Aidha, jumla ya wanafunzi wapya 2,538 walioomba kujiunga na vyuo vya ualimu kwa mwaka wa masomo 2024/2025 wamedahiliwa.

Matokeo ya muda mfupi

- i. Asilimia ya walimu wenye sifa imeongezeka kutoka asilimia 90.45 mwaka 2022 hadi kufikia asilimia 94 mwaka 2023.
- ii. Jumla ya wanafunzi 1,092 wamehitimu mafunzo ya ualimu kwa ngazi ya astashahada na stashahada ya ualimu kwa mwaka 2023 katika Vyuo vya Kiislamu vya Kiuyu Pemba na Mazizini Unguja.
- iii. Programu za mafunzo ya ualimu zimeongezeka kutoka programu 06 mwaka 2022 hadi kufikia programu 07 mwaka 2023.
- iv. Jumla ya walimu 2,778 (1,188 Unguja na 1,590 Pemba) wamepatiwa mafunzo kazini.
- v. Jumla ya walimu wapya 252 (192 Unguja na 60 Pemba) wamepatiwa mafunzo ya awali kazini.

Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti

25. **Mheshimiwa Spika**, Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti ina lengo la kuwaandaa wanafunzi kuingia katika fani

za kitaalamu na ajira. Huduma hii inatolewa katika Vyuo vikuu vitatu vilivyopo Zanzibar ambavyo ni Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Chuo cha Kumbukumbu ya Abdulrahman Al-Sumait na Chuo Kikuu cha Zanzibar (ZU).

26. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kilitengewa ruzuku ya **TSh. 16,610,400,000** kwa ajili ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **TSh. 15,224,263,244** sawa na asilimia **92** zimepatikana. Utekelezaji halisi wa huduma hii ni kama ifuatavyo:-

- i. Mkuu wa Chuo Kikuu Cha Taifa (SUZA) ambae ni Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi alimtunuku Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Samia Suluhu Hassan Shahada ya Heshima ya Uzamivu ya usimamizi wa Utalii na Masoko katika Mahafali ya 19 ya chuo hicho.
- ii. Chuo Kikuu Cha Taifa (SUZA) kimeajiri wafanyakazi wapya 10, kati yao wafanyakazi 8 wanataaluma (6 wanawake na 2 wanaume) na wafanyakazi wawili wanawake wa kada ya Katibu muhtasi. Aidha, jumla ya wafanyakazi 26 wamepewa mikataba ya kuendelea na utumishi kwa ajili ya kupunguza uhaba wa wafanyakazi kati yao 15 ni wazawa (wanaume 8 na wanawake 7) na 11 ni wageni (wanaume 4 na wanawake 7).

- iii. Jumla ya wafanyakazi 128 wapya na wanaoendelea na masomo wamelipiwa ada za masomo katika vyuo na ngazi mbalimbali ikiwemo Shahada ya Uzamivu (PhD) 67, Shahada ya Uzamili (40), Shahada ya kwanza (20) na Stashahada (1).
- iv. Chuo kinaendelea na hatua za awali za kufanya mapitio ya mitaala 6 ili kukidhi vigezo vya TCU.
- v. Chuo kimesaini mkataba na mshauri elekezi kwa ajili ya kupitia michoro na kusimamia ujenzi wa majengo matatu ambayo ni Jengo la Kituo cha Maabara ya Sayansi Asilia, Jengo la Dakhalia za Wanafunzi na Jengo la Maabara za Skuli ya Kilimo ambayo yatajengwa katika kampasi ya Tunguu kupitia mradi wa HEET. Aidha, Chuo kilipokea ugeni kutoka Benki ya Dunia (World Bank Mission) uliokuja kwa lengo la kuangalia maendeleo ya mradi wa HEET na ulizindua gari ya mradi na Kituo cha Kupinga Unyanyasaji wa Kijinsia (Gender Desk Office) kilichopo kampasi ya Tunguu.
- vi. Ujenzi wa uzio wa kampasi ya Tunguu unaendelea ambapo hadi sasa umefikia asilimia 40. Aidha, vibanda viwili vya walinzi vimejengwa katika kampasi ya Tunguu na kimoja katika kampasi ya Kilimani.
- vii. Chuo kimefanya Mkusanyiko wa kwanza wa Kitaaluma (Convocation Day 2023) ambao ulikuwa na lengo la kuwatunuku wahitimu waliofanya vizuri kwenye masomo yao kutoka kila programu sambamba na kuwatunuku

waanzilishi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) (Thinkers and Founders) ambapo Rais wa Mkusanyiko huo alichaguliwa pamoja na kamati zake.

Matokeo ya muda Mfupi

- i. Idadi ya Wanafunzi wanaomaliza ngazi mbalimbali za shahada na stahada imeongezeka kutoka 1,913 mwaka 2023 hadi kufikia 2,102 mwaka 2024.
- ii. Jumla ya wanafunzi 3,562 (wanawake 1,891 na wanaume 1,671) wamedahiliwa katika ngazi mbali mbali.
- iii. Jumla ya programu mbili mpya za masomo zimeanzishwa nazo ni Shahada ya uzamili ya Uongozi wa Biashara katika fedha na Shahada ya kwanza ya Sayansi ya Maabara ya Utabibu.

Huduma ya Sayansi na Teknolojia

27. Mheshimiwa Spika, huduma ya Sayansi na Teknolojia ni miongoni mwa huduma muhimu katika kuinua kiwango cha Elimu ya Uhandisi, Sayansi na Teknolojia na kuimarisha maendeleo ya uchumi wa nchi. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia. Kwa mwaka 2023/2024, Taasisi hii ilitengewa ruzuku ya **TSh. 9,727,200,000**. Kati ya fedha hizo, **TSh. 7,268,000,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za Maendeleo na **TSh. 2,459,200,000** ni kwa ajili ya ruzuku ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2024, Jumla ya **TSh. 2,796,678,299** sawa na

asilimia **29** zilipatikana. Utekelezaji halisi wa shughuli za huduma hii ni kama ifuatavyo:

- i. Jumla ya wafanyakazi 23 wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume wanaendelea na masomo kwenye ngazi mbali mbali zikiwemo Shahada ya Uzamivu (PhD) 7, Shahada ya Uzamili 12, Shahada ya kwanza 3 na Astashahada 1.
- ii. Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume imeingia makubaliano ya mashirikiano na Vyuu na Taasisi za ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kukuza na kuendeleza fani ya sayansi na teknolojia hapa nchini. Miongoni mwa Taasisi za nje ni AP University (Belgium), Nanjing University of Aeronautics and Astronomy (China), Beijing Institute of Technology (BIT) (China), University of Liverpool (UK), Sapienza University (Italy), University of Cyprus, Puma Energy, GFP International (US), IDOM (Spain) na VACE (Austria). Kwa upande wa taasisi za ndani ya nchi Taasisi imefanya makubaliano na Arusha Technical College (ATC), National Institute of Transportation (NIT), VETA na hospitali ya Mnazi Mmoja. Kupitia mashirikiano hayo wafanyakazi na wanafunzi wamekua wakifaidika katika kukuza ujuzi wao wa sayansi na teknolojia.
- iii. Jumla ya wanafunzi wapya 739 (wanaume 596 na wanawake 143) wamesajiliwa katika fani mbalimbali kwa ngazi za Shahada ya kwanza 81, Stashahada 292 na Astashahada ni 366. Wanafunzi waliosoma Skuli

za Ufundi za Kengeja na Mikunguni wanaendelea na masomo yao Taasisi ya Karume- KIST.

- iv. Jumla ya wanafunzi 1,785 wakiwemo wanawake 746 na wanaume 1,039 wanaendelea na masomo katika fani mbalimbali zikiwemo, Shahada ya Uhandisi wa ndege, Shahada ya Uhandisi Ujenzi, Shahada ya Uhandisi Umeme na Elektroniki na Shahada ya “Telecommunication and Network”, Stashahada ya Uhandisi Ujenzi, Stashahada ya teknolojia ya habari mawasiliano na biashara, Stashahada ya Usimamizi wa Maabara, Stashahada ya Mafuta na Gesi, Stashahada ya Umeme na Nishati Jadidifu, Stashahada ya Ufundi Magari, Stashahada ya Ufundi Mitambo, Stashahada ya Elektroniki na Mawasiliano ya Anga, Stashahada ya Uhandisi Kompyuta Stashahada ya Usarifu wa Mazao ya Matunda na Mboga mboga na Usarifu wa Mazao ya Baharini, Stashahada ya Ubunifu wa Maendeleo ya Kidigitali pamoja na mafunzo ya Cheti cha Ufundi Stadi.

Matokeo ya muda Mfupi

- i. Idadi ya wanafunzi 2,619 wameandikishwa katika fani za ufundi, uhandisi, sayansi na Teknolojia mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 4.3 ukilinganisha na matarajio ya wanafunzi 2,510.
- ii. Idadi ya wanafunzi 527 wa fani za ufundi, uhandisi, sayansi na Teknolojia wamehitimu mwaka 2023/2024.

Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu

- 28. Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar inatekeleza majukumu makuu matatu, ambayo ni kutoa mikopo kwa wanafunzi wahitaji wenye sifa za kujiunga na masomo ya elimu ya juu, kusimamia na kufuatilia nafasi za ufadhili wa masomo kutoka kwa washirika mbalimbali wa maendeleo ndani na nje ya Tanzania na kukusanya marejesho ya mikopo ya wanafunzi kutoka kwa wanufaika wote.
- 29. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, jumla ya Tsh. 29,052,900,000 zimetengwa kutekeleza shughuli za huduma hii. Kati ya fedha hizo **Tsh. 9,052,900,000** kwa ajili ya ruzuku ya kazi za kawaida ikiwemo mishahara na **Tsh. 20,000,000,000** za Maendeleo zilitengwa kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wapya na wanaoendelea na masomo ya Elimu ya Juu. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **Tsh. 21,512,117,015** sawa na asilimia **74** zilipatikana. Utekelezaji halisi wa programu hii ni kama ifuatavyo:-
- i. Jumla ya wanafunzi 6,137 wamepatiwa mikopo ya elimu ya juu wakiwemo 2,502 wapya na 3,635 wanaoendelea na masomo. Ongezeko la wanafunzi 77 wapya walioteuliwa inatokana na kuongezeka kwa ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha sita na ongezeko la maombi ya mkopo kwa wanafunzi wapya. Aidha, jumla ya wanafunzi 5 wapya wamepatiwa nafasi za ufadhili wa masomo nje ya nchi kutoka Serikali ya Ufalme wa Ras al-Khaimah.

- ii. Wizara imeendelea kutoa ufadhili wa masomo kupitia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiwa ni zawadi kwa wanafunzi bora waliofaulu vizuri zaidi kwa daraja la kwanza katika mitihani ya Taifa ya Kidato cha Sita katika masomo ya Sayansi, Biashara na Sanaa. Jumla ya wanafunzi 144 wakiwemo wapya 17 na 127 wanaoendelea na masomo wamefaidika na ufadhili huu.
- iii. Jumla ya wanafunzi wapya 54 wamepatiwa ufadhili wa masomo kwa vyuo vya ndani ya nchi wakiwemo 21 wa Chuo Kikuu cha Zanzibar kilichopo Tunguu kupitia ufadhili wa taasisi za Darul Iman. Aidha, wanafunzi 33 wa Chuo Kikuu cha Abdulrahman Al – Sumait cha Chukwani walipatiwa ufadhili kupitia Shirika la “Direct Aid” (African Muslim Agency).
- iv. Jumla ya wanafunzi 1,605 wakiwemo wanafunzi 901 wanaosoma vyuo vya Zanzibar, 611 wa vyuo vya Tanzania Bara na 93 wa vyuo vya nje ya Tanzania wanatarajiwa kuhitimu masomo yao katika fani na ngazi mbali mbali za elimu ya juu.

Matokeo ya muda Mfupi

- i) Idadi ya Wanafunzi 6,137 wamepatiwa mikopo ya Elimu ya juu katika vyuo mbalimbali sawa na ongezeko la asilimia 1.2 kulinganisha na matarajio ya wanafunzi 6,060 waliotarajiwa kupatiwa mikopo hiyo.
- ii) Hadi kufikia Aprili 2023, jumla ya TSh 3,440,000,000/- zimekusanywa sawa na asilimia 84 ya lengo lililowekwa.

Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu

30. Mheshimiwa Spika, huduma hii ina jukumu la kusimamia na kutathmini maendeleo ya elimu ya juu na inatekelezwa na Kitengo cha Uratibu wa Elimu ya Juu. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Kitengo kilitengewa jumla ya **Tsh. 70,000,000** kutoka Serikalini. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **Tsh. 53,321,850** sawa na asilimia **76** zimepatikana. Utekelezaji halisi ni kama ifuatavyo:-

- i. Kitengo cha Uratibu wa Elimu ya juu kimefanya ufuatiliaji na tathmini katika vyuo vikuu 3 na vyuo 18 vya kati kuangalia utoaji wa Elimu na uendeshaji katika Taasisi hizo pamoja na kusikiliza na kutatua changamoto mbalimbali za wanafunzi wanazokutana nazo Vyuoni.
- ii. Kitengo kimefanya maonesho ya 4 ya Wiki ya Elimu ya Juu kwa lengo la kutoa Elimu na miongozo kwa wadau wote wa Elimu pamoja na wanafunzi wanaomaliza kidato cha sita ambao wanatarajiwa kujiunga na Elimu ya Juu. Jumla ya washiriki 54 walipata fursa ya kuonesha kazi zao na jumla ya wadau 19,121 walitembelea katika mabanda ya maonesho hayo.
- iii. Kitengo kimefanya kongamano kwa wanafunzi wanawake wa Vyuo Vikuu waliojiunga na Elimu ya Juu Zanzibar kwa mwaka 2023/2024 juu ya athari za mfumo mbaya wa maisha wanayoishi wakiwa Vyuoni ambao unatoka nje ya mila, silka na desturi za Wazanzibari. Jumla ya Taasisi 13 zimeshiriki na wanafunzi wakike

285 wamepatiwa Elimu ya Kujitambua na Kujiamini, Elimu ya Kiafya na Elimu ya Dini.

- iv. Wizara kupitia Kitengo cha Uratibu wa Elimu ya Juu imetangaza nafasi za masomo za ndani na nje ya nchi ya Tanzania masomoni. Nafasi za masomo zilizotangazwa kwa mwaka 2023 - 2024 ni kutoka nchi 10 za wahisani zikiwemo Algeria, Jumuiya ya Madola, Swiss, Hungary, China, Morocco, Mauritius, Misri, Indonesia, na Uturuki, kwa ngazi za Shahada ya kwanza, ya pili na ya tatu katika fani za Udaktari, Uchumi, Ukandarasi, Uwalimu, Uuguzi na Sayansi ya Mazingira, Kilimo, Usimamizi wa Biashara na Utawala, Siasa na Uhusiano wa Kimataifa, Maendeleo ya Jamii, na Sayansi ya TEHAMA.
- v. Jumla ya waombaji 186 (114 wanaume na 72 wanawake) wa nafasi za masomo zilizotangazwa waliwasilisha maombi, ambapo wanafunzi 14 walipata ufadhili; China ni wanafunzi 8, Algeria wanafunzi 5, Misri mwanafunzi 1 na majibu ya nchi nyengine bado hayajatoka. Aidha, wanafunzi 2 wanaume waliripoti kutoka masomoni katika fani ya "Science in Transportation Engineering and Information Technology".

Matokeo ya muda mfupi

- i. Jumla ya wanafunzi 12,306 wanaendelea na masomo ya Elimu ya Juu wakiwemo wanawake 7,468 na wanaume 4,838.

- ii. Jumla ya wahitimu 3,218 (wanawake 1,863 na wanaume 1,355) wamehitimu masomo ya Elimu ya juu kutoka katika vyuo vitatu SUZA, ZU na Chuo cha Kumbukumbu ya Abdulrahman Al-Sumait.

PROGRAMU YA NNE: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI

- 31. Mheshimiwa Spika**, programu hii ina madhumuni ya kuwajengea vijana uwezo katika ushindani wa soko la ajira kwa kuwapatia mafunzo ya amali na mbadala. Programu hii ina programu ndogo mbili; Mafunzo ya Amali na Elimu Mbadala na Watu Wazima. Programu ilitengewa jumla ya **TSh. 37,028,642,302**. Katiya fedhahizo, **TSh. 10,044,175,302** ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida ikiwemo **TSh. 4,133,075,302** kwa ajili ya malipo ya mishahara, **TSh. 5,911,100,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 26,984,467,000** ni kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **TSh. 8,030,057,479** sawa na asilimia **22** zilipatikana.

Programu ndogo ya Mafunzo ya Amali

- 32. Mheshimiwa Spika**, programu hii ndogo ilitengewa jumla ya ruzuku ya **TSh. 35,615,167,000** Kati ya fedha hizo, **TSh. 8,630,700,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida ikiwemo **Tsh. 3,247,600,000** kwa ajili ya mishahara, **TSh. 5,383,100,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 26,984,467,000** ni kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **TSh. 6,950,070,470** sawa na

asilimia 20 zilipatikana. Utekelezaji halisi wa programu hii ni kama ifuatavyo:-

- i. Wizara inaendelea kufanya manunuzi ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ajili ya Chuo cha Mkokotoni na Daya. Miongoni mwa vifaa hivyo ni vifaa vya fani ya mapokezi (Front Office) na Utunzaji wa Nyumba (House Keeping).
- ii. Wizara imeadhimisha Wiki ya Mafunzo ya Amali iliyofanyika Disemba 2023 katika viwanja vya Mnara wa Kumbukumbu Kisonge. Shughuli mbalimbali zilifanywa zikiwemo maonesho ya bidhaa zinazozalishwa vyuoni, maonesho ya mavazi, bonanza la michezo, matembezi ya hiyari pamoja na uchangiaji damu.
- iii. Jumla ya vituo saba (7) kati ya vituo kumi na sita (16) vilivyopangwa kupatiwa usajili vimepatiwa usajili kutokana na kukidhi vigezo.
- iv. Timu ya ukaguzi ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali imefanya ufuatiliaji na ukaguzi wa vyo 23, vikiwemo Chuo cha Amali Mkokotoni, Mwanakwerekwe, Makunduchi, Capital Technology Center, Adult Training Center, ZAMONA, ZENITH na KAWA kwa upande wa Unguja, Daya, Vitongoji, Samail Vocational Training Center, Center for Professional and Vocational Training, Wete Vocational Training Center, Wingwi Adult Vocational Training Center kwa upande wa Pemba.

- v. Wizara kupitia Mamlaka ya Mafunzo ya Amali imeandaa na kuratibu mtihani wa Taifa wa Mafunzo ya Amali. Jumla ya watahiniwa 2,594 (wanawake 1,161 na wanaume 1,433) kutoka katika vituo 17 vya Mafunzo ya Amali vya serikali na binafsi walifanya mtihani huo. Aidha, Mamlaka imeviwezesha vituo vyake kwa kuvipatia malighafi kwa ajili ya mtihani wa vitendo.
- vi. Wizara imeanza maandalizi ya kuanzisha fani mpya kulingana na soko la ajira na Uchumi wa Buluu. Aidha, Jumla ya wakufunzi na wafanyakazi 7 wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya shahada ya kwanza ya fani za uhandisi na shahada ya pili katika Mipango. Aidha wakufunzi 28 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika vyuo mbalimbali nchini.
- vii. Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kupitia Chuo cha Daya na Mkokotoni imetoa mafunzo kwa wanafunzi 150 wa fani za muda mfupi za upishi, utunzaji wa nyumba, mapokezi na huduma ya chakula na vinywaji.

Matokeo ya muda mfupi

- i. Jumla ya vikundi 28 vya wahitimu wa Mafunzo ya Amali wamepatiwa mikopo na kujajiri kwa mwaka 2024.
- ii. Idadi ya wanafunzi 2,217 wakiwemo wanafunzi wa mafunzo ya muda mfupi wamejiunga katika vyuo vya mafunzo ya amali.
- iii. Jumla ya wanafunzi 860 wamehitimu mafunzo katika vyuo vya amali mwaka 2023.

Programu ndogo ya Elimu Mbadala na Watu Wazima

33. Mheshimiwa Spika, programu hii inatekelezwa na Idara ya Elimu Mbadala na Watu Wazima na ina lengo la kupunguza kiwango cha wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu kwa wanajamii. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, programu hii ilitengewa jumla ya **TSh. 1,413,475,302** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo **TSh. 885,475,302** ni kwa ajili ya mishahara na **Tsh. 528,000,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **TSh. 1,079,987,009** sawa na asilimia **76** zilipatikana. Utekelezaji halisi wa shughuli za programu hii ni kama ifuatavyo:-

- i. Jumla ya wanafunzi 2,235 wakiwemo wanawake 619 na wanaume 1,616 wamesajiliwa kujiunga na madarasa ya Elimu Mbadala Unguja na Pemba. Aidha madarasa ya Elimu Mbadala yameongezeka kutoka 98 mwaka 2022 na kufikia 104 (Unguja 50 na Pemba 54) mwaka 2023.
- ii. Maadhimisho ya wiki ya Elimu ya watu wazima yamefanyika ambapo wanakisomo 392, kati ya hao wanawake ni 358 wamepata fursa ya kujipima uwezo wa kusoma vitabu, magazeti na majarida mbalimbali.
- iii. Jumla ya vikundi vya wanakisomo 59 (17 Unguja, 42 Pemba) vyenye idadi ya wanachama 1,125 wakiwemo wanawake 1,013 na wanaume 112 vimeendelezwa kwa lengo la kuwapunguzia wanakisomo utegemezi na umasikini wa kipato.

Matokeo ya muda mfupi

- i. Jumla ya wanafunzi 31,639 (wanaume 16,310 na wanawake 15,329) wenye umri kati ya miaka 7 hadi 14 waliokuwa nje ya skuli wamerejea skuli kuendelea na masomo Unguja na Pemba katika kipindi cha Miaka mitatu ambao sawa na asilimia 88.5 ya shabaha ya kuwarejesha watoto 35,732.
- ii. Jumla ya wanakisomo 6,001 wameandikishwa katika madarasa ya kisomo wakiwemo wanaume 682 na wanawake 5,319 kwa Unguja na Pemba.
- iii. Jumla ya wanafunzi 736 (wanaume 356 na wanawake 380) wenye umri kati ya miaka 15 hadi 22 wameandikishwa katika kituo cha elimu mbadala Rahaleo Unguja na kituo cha Wingwi Mtemani Pemba.

PROGRAMU YA TANO: UBORA WA ELIMU

34. Mheshimiwa Spika, programu hii ina lengo la kuhakikisha elimu inayotolewa katika ngazi zote inaleta manufaa kwa mwenye kuhitimu, jamii na taifa kwa ujumla. Programu hii ilitengewa jumla ya **TSh. 12,495,809,878**, Kati ya fedha hizo, **TSh 6,075,882,457** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 6,419,927,421** ni kwa ajili ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **TSh. 11,415,996,735** sawa na asilimia 91 zilipatikana. Programu hii ina jumla ya programu ndogo tatu na maeneo matano ya kutoa huduma kama ifuatavyo:-

Huduma ya Mitaala na Vifaa vya Kufundishia

35. Mheshimiwa Spika, Huduma hii ina madhumuni ya kutayarisha mitaala ya elimu na kuratibu upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ngazi za elimu ya maandalizi, msingi, Sekondari na mafunzo ya Ualimu. Shughuli za utoaji wa huduma hii zinatekelezwa na Taasisi ya Elimu Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Taasisi ilitengewa ruzuku yenye jumla ya **TSh. 1,640,800,000**. Kati ya fedha hizo, **TSh. 358,100,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 1,282,700,000** ni kwa malipo ya mishahara. Hadi kufikia Aprili, 2024, jumla ya **TSh. 1,424,536,753** sawa na asilimia **87** zilipatikana. Utekelezaji halisi wa huduma hii ni kama ifuatavyo:-

- i. Wizara imefanya ufuatiliaji katika skuli 90 za maandalizi na msingi (63 Unguja na 27 Pemba) kuhusu matumizi ya mtaala mpya katika madarasa ya maandalizi mwaka wa I, darasa la I, IV na VII ambayo yalianza kutekeleza mtaala mpya. Ripoti inaonesha kuwa zaidi ya asilimia 80 ya walimu wanaofundisha madarasa hayo walipatiwa mafunzo ya matumizi ya mtaala mpya.
- ii. Wizara imefanya uhamasishaji kwa jamii kuhusu mabadiliko ya mitaala kwa ngazi za elimu ya maandalizi, msingi na Sekondari kupitia vyombo vya habari, ambapo programu mbalimbali za elimu ya mabadiliko ya mitaala zilifanyika na kurushwa katika vyombo vinane vya habari vya Unguja na Pemba. Kupitia programu hizi, sehemu kubwa ya jamii na wadau wengine zikiwemo skuli binafsi, wazazi na

waandishi wa vitabu wanafahamu mabadiliko ya mitaala yaliyopo.

- iii. Jumla ya watumishi 48 wa Taasisi ya Elimu Zanzibar wamepatiwa mafunzo, kati yao watumishi 20 walipatiwa mafunzo kuhusu matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa manunuzi (e-procure) na watumishi 28 mafunzo kuhusu matumizi ya mfumo wa masjala mtandao (e-office).

Matokeo ya muda mfupi

- i. Mtaala mpya wa elimu ya maandalizi na msingi umeanza kutumika katika skuli zote za Serikali na binafsi kwa madarasa ya maandalizi 1, Darasa la 1, Darasa la 4 na Darasa la 7.
- ii. Jumla ya vitabu vya wanafunzi 1,130,676 na viongozi vya mwalimu 248,000 vilichapishwa kwa ajili ya utekelezaji wa mtaala mpya wa umahiri mwaka 2023 vikiwemo vya Wanafunzi wenye mahitaji maalum. Aidha, jumla ya vitabu 656,493 vimesambazwa katika skuli 662 za Serikali Unguja na Pemba.
- iii. Jumla ya walimu 6,457 wa skuli za Serikali na binafsi wamepata mafunzo ya matumizi ya mtaala mpya kuweza kufundisha kwa umahiri.

Huduma ya Upimaji na Tathmini ya Elimu

- 36. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina madhumuni ya kupima na kutathmini utoaji wa elimu. Shughuli za huduma hii

zinatekelezwa na Baraza la Mitihani la Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, huduma ya Upimaji na Tathmini ilitengewa ruzuku ya **TSh. 5,028,100,000**. Kati ya fedha hizo, **TSh. 3,837,200,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 1,190,900,000** ni kwa ajili ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **TSh. 5,531,536,883** sawa na asilimia **110** zilipatikana. Ongezeko hili lilitokana na ongezeko la gharama za mitihani ukilinganisha na bajeti iliyotengwa. Utekelezaji halisi wa shughuli za huduma ya Upimaji na Tathmini ni kama ifuatavyo:-

- i. Jumla ya wanafunzi 58,664 wa Darasa la Nne (wanaume 29,950 na wanawake 28,714) sawa na asilimia 95.98, wanafunzi 44,726 wa Darasa la saba (wanaume 21,465 na wanawake 23,261) sawa na asilimia 97.42 na wanafunzi 24,391 (wanaume 10,565 na wanawake 13,826) sawa na asilimia 96.69 wa Kidato cha Pili waliandikishwa kufanya Mtihani.
- ii. Jumla ya walimu tarajali 890 (wanaume 72 na wanawake 818) waliandikishwa kufanya mtihani ya Cheti cha Ualimu Maandalizi, ambapo wanafunzi 881 sawa na asilimia 99. wamefanya Mtihani huo.
- iii. Baraza la Mitihani limewaandikisha Walimu tarajali 590 (102 wanaume na 488 wanawake) wanaotarajiwa kufanya Mitihani ya kumaliza masomo ya Stashahada ya Msingi ya Ualimu katika Vyuo mbali mbali vya serikali na binafsi Unguja na Pemba, Mitihani hiyo inatarajiwa kufanyika kuanzia tarehe 20–29 Mei, 2024.

Matokeo ya Muda Mfupi

- i. Jumla ya wanafunzi 50,897 sawa na asilimia 90.39 walifaulu mtihani wa Darasa la Nne, kati ya hao, wanaume ni 24,753 sawa na asilimia 48.63 na wanawake ni 26,144 sawa asilimia 51.37 ya watahiniwa wote.
- ii. Jumla ya wanafunzi 41,396 wa Darasa la Saba sawa na asilimia 95.00 walifaulu mtihani ambapo wanaume ni 18,966 sawa na asilimia 45.82 na wanawake ni 22,430 sawa na asilimia 54.18. Aidha, wanafunzi 6,666 sawa na asilimia 15.30 wamefaulu kuendelea na masomo yao katika madarasa ya Michepuo na Vipawa.
- iii. Kwa upande wa kidato cha pili Wanafunzi 21,489 sawa na asilimia 91.12 wamefaulu Mtihani huo na kuendelea na masomo ya Kidato cha Tatu wakiwemo wanaume 8,579 sawa na asilimia 39.92 na wanawake 12,910 sawa na asilimia 60.08
- iv. Aidha, Wanafunzi 844 sawa na asilimia 95.80 wamefaulu mtihani wa Cheti cha Ualimu Maandalizi (CECE) ambapo wanaume ni 68 sawa na asilimia 8.06 na wanawake ni 776 sawa na asilimia 91.94.

Huduma ya Ukaguzi wa Elimu

37. Mheshimiwa Spika, huduma hii ina madhumuni ya kusimamia ubora wa elimu itolewayo kwa kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa inafuata sera, sheria, miongozo na taratibu zilizopo. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu. Kwa mwaka wa fedha

2023/2024, huduma hii ilipangiwa jumla ya ruzuku ya **TSh. 2,650,200,000**. Kati ya fedha hizo, **TSh. 487,500,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 2,162,700,000** ni malipo ya mishahara ya wafanyakazi. Hadi kufikia Aprili, 2024, jumla ya **TSh. 2,006,770,048** sawa na asilimia **76** zilipatikana. Utekelezaji wa shughuli za huduma hii ni kama ifuatavyo:-

- i. Jumla ya walimu 2,213 wamekaguliwa kati ya 2,800 sawa na asilimia 79 na kupewa ushauri kulingana na masomo wanayofundisha, ushauri huu umezingatia ufundishaji wa mtaala wa umahiri, upimaji endelevu kwa wanafunzi, matumizi ya mbinu sahihi na vifaa, uhuishaji wa paneli za masomo, utoaji mrejesho kwa kazi za wanafunzi na ukamilishaji wa mada katika mihutasari. Aidha, Mafunzo ya matumizi ya Muongozo wa ukaguzi yametolewa kwa wakaguzi wapya 14 kwa lengo la kuwawezesha kufanya kazi zao kwa ufanisi.
- ii. Jumla ya wakaguzi na watendaji 102 wa Ofisi ya Mkaguzi wa Elimu walishiriki katika mafunzo ya kuwajengea uelewa juu ya mtaala unaozingatia umahiri. Mafunzo hayo yamehusisha utungaji wa maswali yanayopima mtaala huo pamoja na mbinu za ufundishaji.
- iii. Jumla ya watendaji wawili wa Ofisi wamelipiwa ada za masomo katika Chuo Kikuu cha Zanzibar na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania katika ngazi ya shahada ya kwanza na ya tatu. Aidha mafunzo ya muda mfupi yametolewa kwa watendaji wawili katika chuo cha IPA na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA).

- iv. Jumla ya wafanyakazi 109 wa Ofisi ya Mkaguzi wa Elimu Unguja na Pemba wamepatiwa mafunzo ya matumizi ya Kompyuta pamoja na matengenezo madogo madogo kwa lengo la kuzitunza kompyuta hizo.
- v. Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu imefanya upimaji kwa wanafunzi 1,803 wa darasa la Pili katika skuli 95 za Unguja na Pemba. Matokeo ya upimaji huo yanaonesha kuwa asilimia 65 ya wanafunzi hao wamefanya vizuri katika somo la kiswahili kipengele cha kusoma kwa ufahamu na uandishi wa Imla. Kwa upande wa somo la hisabati asilimia 60 ya wanafunzi hao wanahitaji msaada zaidi katika kujumlisha na kutoa.

Matokeo ya Muda Mfupi

- i. Jumla ya skuli 765 zimekaguliwa (575 za Serikali na 190 za Binafsi) kati ya skuli 980 sawa na asilimia 78 ya makadirio ya skuli zilizopangwa kukaguliwa kwa Unguja na Pemba mwaka 2023/2024.

Huduma za Maktaba

38. Mheshimiwa Spika, Programu hii ina madhumuni ya kutoa fursa ya kutumia vitabu, nyaraka na nyenzo nyengine za taaluma kwa watoto, wanafunzi wa ngazi zote na jamii. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Bodi ya Huduma za Maktaba Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2023-2024 huduma hii ilipangiwa kutumia ruzuku ya **TSh. 1,065,600,000**. Kati ya fedha hizo **TSh. 741,200,000** ni kwa ajili ya mishahara na **TSh. 324,400,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia

Aprili 2024 jumla ya **TSh. 804,471,996** sawa na asilimia **75** zilipatikana. Utekelezaji halisi wa shughuli za huduma hii ni kama ifuatavyo:-

- i. Jumla ya maktaba 5 za skuli za msingi za Kizimkazi, Mfenesini, Kitogani, Kiyongwe kwa Unguja na skuli ya Uwandani kwa Pemba zimeimarishwa na kupatiwa vitendea kazi.
- ii. Jumla ya vitabu nane vya nukta nundu vimenunuliwa kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalum, na vitabu 21,643 vimepokelewa kutoka shirika la kimataifa la Uingereza la Book Aid International, vitabu 200 vya Kiswahili vimepokelewa kutoka SAFAL ALAF FOUNDATION, nakala 2,833 za magazeti zimenunuliwa pamoja na vifaa vya kielektroniki kwa ajili ya maktaba mtandao (e-library).
- iii. Jumla ya wafanyakazi 04 na wakutubi 02 wamepatiwa mafunzo ya mifumo ya TEHAMA, Ukutubi na utoaji wa huduma za maktaba, manunuzi na uhasibu. Aidha, Programu 156 ziliendeshwa katika maktaba zikijumuisha watoto, wanafunzi wa msingi na Sekondari pamoja na programu za vijana.

Matokeo ya Muda Mfupi

- i. Idadi ya wanachama wapya waliosajiliwa imefikia jumla 562 kati yao wanaume 247 wanawake 315
- ii. Idadi ya watumiaji wa maktaba imefikia 30,942 kati ya hao wanaume 17,061 na wanawake 13,881

Huduma ya Urajisi wa Elimu

39. Mheshimiwa Spika, huduma hii ina madhumuni ya kuhakikisha sheria, sera na taratibu za Wizara zinafuatwa katika skuli za Serikali na za Binafsi. Huduma hii pia inatoa leseni kwa walimu na kuzisajili skuli za Serikali na za Binafsi pamoja na vyuo vya ualimu vya kati. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Afisi ya Mrajisi wa Elimu. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, huduma hii ilipangiwa kutumia jumla ya ruzuku ya **TSh. 319,400,000**. Kati ya fedha hizo, **TSh. 90,800,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 228,600,000** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara ya wafanyakazi. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **TSh. 304,517,845** sawa na asilimia **95** zimepatikana. Utekelezaji halisi wa huduma hii ni kama ifuatavyo:-

- i. Jumla ya skuli 526 za ngazi mbali mbali za Serikali na Binafsi zimehakikiwa Unguja na Pemba (361 Unguja na 165 Pemba). Aidha, vyuo vya Ualimu vya Binafsi 16 (10 Unguja na 6 Pemba) vimepatiwa usajili na vyuo viwili vilivyomba usajili katika mwezi wa Disemba 2023, kwa ngazi ya Cheti na Diploma ya Ualimu vimefanyiwa ufuatiliaji.
- ii. Jumla ya walimu wapya 1,433 wa ngazi ya cheti, stashahada, shahada ya kwanza na ya pili wamepatiwa leseni za kufundishia za muda wa miaka mitano (5) kutoka skuli za Serikali na Binafsi. Aidha, jumla ya walimu 702 ambao hawajasomea wamepatiwa leseni za kufundishia za muda wa mwaka mmoja (1). Walimu hawa wanatakiwa kuomba vyuo mbalimbali ili kupewa mafunzo ya ualimu.

- iii. Zoezi la utoaji wa leseni mpya za walimu kwa kutumia mfumo wa kielektroniki linaendelea, jumla ya walimu 1,105 (wanawake 799 na wanaume 306) taarifa zao zimeshaingizwa katika mfumo na wamepatiwa leseni za elektroniki.
- iv. Wizara imewapatia wanafunzi 64 (16 Unguja na 48 Pemba) ambao walipata ujauzito na kurejea skuli msaada wa vifaa vya kujifunzia pamoja na mahitaji ya watoto wao.
- v. Jumla ya kesi 6 (1Unguja na 5 Pemba) za udhalilishaji zikiwemo ubakaji, ulawiti zimeripotiwa katika ofisi ya Mrajis wa Elimu na kwa sasa Wizara inazifuatilia.

Matokeo ya muda mfupi

- i. Jumla ya skuli 71 za Unguja na Pemba za binafsi zimesajiliwa. Kati ya skuli hizo 25 za maandalizi, skuli 2 za maandalizi, skuli 44 za maandalizi na msingi, na Sekondari zimepatiwa usajili wa muda.

Programu ndogo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu

40. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina madhumuni ya kuifanya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano itumike katika ngazi ya utawala, kujifunza na kufundishia, kuimarisha huduma ya mawasiliano na kutunza usalama wa taarifa. Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya **TSh.**

871,065,878. Kati ya fedha hizo, **TSh. 300,000,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 571,065,878** ni kwa malipo ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **TSh. 521,579,954** ambazo ni sawa na asilimia **60** zimepatikana. Utekelezaji halisi wa programu hii ni kama ifuatavyo:-

- i. Jumla ya Skuli 5 (2 za msingi na 3 za Sekondari) zimeungwa na mkonga wa Taifa. Aidha, kwa kuzingatia umuhimu wa teknolojia katika elimu, Wizara imezipatia vifaa vya TEHAMA na kuunganisha mfumo wa Mtandao (Local Area Network) katika skuli 11.
- ii. Wizara kupitia Idara ya TEHAMA katika Elimu imefanya ziara za ufuatiliaji wa matumizi ya vifaa vya TEHAMA pamoja na kuchambua changamoto na matatizo yanayokabili vifaa vya TEHAMA katika skuli ya Fuoni Sekondari, Skuli ya Sekondari Mombasa Biashara, Skuli ya Sekondari ya Ufundi Mikunguni na Skuli ya Sekondari Hasnuu Makame. Aidha, maandalizi ya kufanya uchambuzi wa kuangalia jinsi ya kuweza kukuza matumizi ya TEHAMA katika kufundishia na kujifunzia katika Vituo vitano ya walimu (TC) yanaendelea.
- iii. Jumla ya wafanyakazi 9 wa Idara ya TEHAMA wamepatiwa mafunzo ya kukuza ujuzi, wafanyakazi 4 wamepatiwa mafunzo ya “Server management”, 4 wamepatiwa mafunzo ya “System Administration” na mfanyakazi 1 kapatiwa mafunzo ya udereva.
- iv. Wizara kupitia Idara ya TEHAMA katika Elimu inaendelea kuimarisha Maudhui ya kidijitali ya Mfumo wa Elimu wa

wanafunzi kuweza kujitathmini wao wenyewe (ZEAS) mfumo huu utawasaidia wanafunzi kujibu maswali na kupata majibu wakiwa nyumbani, Jumla ya masomo 15 yameingizwa katika mfumo huo yakiwemo masomo ya darasa la Saba na Kidato cha Pili.

- v. Wizara kupitia Kituo cha Habari katika Elimu Kwarara (KMEC) imeandaa programu 22 za televisheni vya lugha ya alama kwa wanafunzi wa maandalizi na msingi, programu hizi zimejikita katika masomo ya Hisabati, Kiswahili, Historia Pamoja na stadi za Maisha. Lengo la programu hizi ni kuwasidia walimu na wanafunzi wenye mahitaji maulum kwa upande wa usikivu hafifu ili kufahamu mambo mbali mbali katika masomo yao.
- vi. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mufti imeandaa vipindi 22 vya televisheni vinavyoitwa Jabal Hira, vipindi hivi vina lengo la kuwasaidia walimu na wanafunzi kujifunza mambo mbali mbali ya Dini ya Kiislam hasa kwa upande wa masomo ya wanafunzi darasani na kuwawezesha kujibu vyema mitihani yao ya taifa
- vii. Wizara imeandaa programu 12 za chemsha bongo (Happy Edu Quiz) kwa wanafunzi wa skuli za Sekondari za Serikali na Binafsi kwa masomo ya Sayansi, Hesabu pamoja na Kiingereza.
- viii. Wizara kwa ushirikiana na Shirika la kuhudumia watoto Ulimwenguni ilishiriki kuandaa maonesho ya program za stadi za maisha kwa wanafunzi zinazojulikana kama

KIJANA AMKA ambazo zilikuwa na lengo la kuonesha changamoto wanazokabiliana nazo wanafunzi pamoja na suluhisho.

Matokeo ya muda mfupi

- i. Idadi ya walimu waliopatiwa ujuzi wa TEHAMA kwa mwaka imeongezeka kutoka walimu 86 mwaka 2022/2023 hadi kufikia walimu 223 mwaka 2023/2024. Hii ni sawa na asilimia 55.7 ya matarajio ya walimu 400.

Programu ndogo ya Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha

- 41. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa elimu kwa watoto wote wakiwemo wenye mahitaji maalum. Programu hii inatekelezwa na Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 programu hii ilitengewa jumla ya **TSh. 150,000,000** kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Aprili, 2024, jumla ya **TSh. 72,819,000** sawa na asilimia **49** zilipatikana. Utekelezaji halisi wa shughuli za programu hii ndogo ni kama ifuatavyo:-

- i. Wizara imefanya ufuatiliaji wa kazi katika skuli 25 za Msingi na Sekondari kwa lengo la kuangalia masuala ya Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha pamoja na kuwatambua wanafunzi wenye mahitaji maalumu na kuwapatia vifaa vikiwemo viti vya maringi mawili, mashine za nukta nundu, karatasi za kuandikia maandishi ya nukta nundu, mashine 2 za kurikodia sauti (voice recorder).

- ii. Wizara ya Elimu wakishirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka wamefanya ufuatiliaji kwa waathirika wa masuala ya ukatili wa kijinsia, aidha jumla ya waathirika 25 (wanawake 19 wanaume 6) wa ukatili wa kijinsia Unguja na Pemba walifuatiliwa na kupata taarifa juu ya namna wanavyoendelea kiafya, kitaaluma, kisaikolojia na kijamii. Aidha, jumla ya wanafunzi 50 (23 wanaume 27 wanawake) wa Skuli ya Jang’ombe Msingi wamepatiwa elimu kuhusu athari za madawa ya kulevya ikiwemo matumizi ya shisha.
- iii. Wizara imefanya mkutano na wazazi 144 (wanawake 118 na wanaume 26) wa skuli ya Ghana msingi iliyoko katika Wilaya ya Kati kuhusu malezi na athari za udhalilishaji wa wanafunzi. Aidha, jumla ya wanafunzi 390 (181 wanaume, 209 wanawake) wa klabu za TUSEME wa skuli 30 za Msingi (18 Unguja 12 Pemba) wamepatiwa mafunzo ya klabu za TUSEME kuhusu Elimu ya Stadi za Maisha itakayowawezesha kujitambua na kujiwekea malengo na kuyafikia kwa ufanisi.
- iv. Jumla ya wanafunzi 222 (wanaume 60 na wanawake 162) wa Vituo vya Amali wamepatiwa Elimu ya Stadi za Maisha yenye lengo la kuwasaida waweze kupambana na changamoto zinazowakabili.

Matokeo ya muda mfupi

- i. Jumla ya walimu 1,034 (772 wanawake na 262 wanaume) wamepatiwa mafunzo ya elimu mjumuisho na stadi za maisha.

Programu ndogo ya Michezo na Utamaduni

42. Mheshimiwa Spika, Programu hii ina madhumuni ya kumuandaa mwanafunzi kimwili, kiafya na kiakili katika kujifunza kwa kupitia michezo. Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Michezo na Utamaduni katika elimu. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya **TSh. 770,644,000**. Kati ya fedha hizo, **TSh. 527,882,457** ni kwa matumizi mengineyo na **TSh. 242,761,543** ni kwa ajili ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **TSh. 749,764,256** sawa na asilimia **97** zilipatikana. Utekelezaji wa programu hii ni kama ifuatavyo:-

- i. Wizara imefanikiwa kuadhimisha miaka 59 ya Elimu bila Malipo. Maadhimisho hayo yalianza kwa mashindano ya michezo na sanaa kuanzia ngazi ya Skuli, Wilaya, Mkoa hadi Taifa. Aidha, katika maadhimisho hayo yamefanyika maonesho ya kitaaluma, makongamano ya michezo na uzinduzi wa miradi mbalimbali.
- ii. Jumla ya walimu 44 wa michezo kutoka Wilaya zote za Uguja na Pemba wamepatiwa mafunzo ya ukocho wa mpira wa miguu na walimu 30 wamepatiwa mafunzo ya RIADHA na JUIJITSU
- iii. Wizara kwa kushirikiana na Chama cha Baseball Tanzania imetoa mafunzo ya Baseball kwa walimu 16 na maafisa 2 wa Idara ya Michezo na Utamaduni katika Elimu. Aidha, Wizara imeendeleza mashirikiano na Chama cha Skauti Tanzania (TSA) ambapo jumla ya walimu 6 wamepatiwa mafunzo ya Matron.

- iv. Wizara kupitia Idara ya Michezo na Utamaduni kwa kushirikiana na “The Panje Project” imetoa mafunzo ya kuogelea kwa wanafunzi 57,320 wa Msingi na Sekondari kwa Nadharia Unguja na Pemba na wanafunzi 1,996 walipatiwa mafunzo ya kuogelea kwa vitendo.

Matokeo ya muda mfupi

- i) Ushindani na ushiriki wa michezo na sanaa katika ngazi ya kikanda na kitaifa umefanikiwa kwa kushinda vikombe zaidi ya 6 katika michezo ya Mpira wa Miguu, Mpira wa Mikono, Riadha, Mpira wa Wavu, Mpira wa Meza na Mpira wa Kikapu.
- ii) Kwa mwaka 2023/2024 mashindano ya michezo mbali mbali na sanaa yamefanyika katika ngazi ya kanda na Kitaifa. Aidha jumla ya wanafunzi 311 wenye vipaji vya michezo, Sanaa na utamaduni wameshiriki katika michezo hiyo.
- iii) Idadi ya walimu 437 wamepatiwa taaluma ya michezo, Sanaa na utamaduni. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 45 la matarajio ya walimu 300 waliopangwa kupatiwa mafunzo.
- iv) Jumla ya skuli 20 za msingi na Sekondari zimepatiwa vifaa vya michezo mbali mbali. Hii ni sawa na asilimia 66.6 ya matarajio ya skuli 30 zilizopangwa kupatiwa vifaa.

PROGRAMU YA SITA: UTAWALA NA UONGOZI

43. Mheshimiwa Spika, Programu ya Utawala na Uongozi ina lengo la kuhakikisha usimamizi wa matumizi na upatikanaji wa rasilimali bora katika utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya elimu. Programu hii ina programu ndogo tatu zikiwemo Programu ndogo ya Uongozi kwa ujumla, Programu ndogo ya shughuli za Mipango, Sera na Utafiti na Programu ndogo ya uratibu wa shughuli za Elimu Pemba. Programu hii ilipangiwa jumla ya **TSh. 26,424,971,277**. Kati ya fedha hizo, **TSh. 9,564,682,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **TSh. 9,648,249,277** ni kwa ajili ya mishahara na **TSh. 7,212,040,000** ni kwa ajili ya kazi za Maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **TSh. 14,102,787,494** sawa na asilimia **53** zilipatikana.

Programu ndogo ya Uongozi kwa Ujumla

44. Mheshimiwa Spika, programu hii ina madhumuni ya kuhakikisha ufanisi wa Uongozi na Utawala wa rasilimali za Wizara. Shughuli za programu hii ndogo zinatekelezwa na Idara ya Utumishi na Uendeshaji. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, programu hii ilipangiwa jumla ya **TSh. 11,658,958,000**. Kati ya fedha hizo, **TSh. 6,251,182,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TSh. 5,407,776,000** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **TSh. 10,537,030,611** sawa na asilimia **90** zilipatikana. Utekelezaji wa kazi za programu hii ni kama ifuatavyo:-

- i) Jumla ya wafanyakazi 374 (Pemba 309 na Unguja 65) wamelipwa posho la likizo lenye thamani ya Tshs 37,400,000. Aidha, wafanyakazi 750 wamelipwa stahiki yao ya ubani wa ufiwa na wafanyakazi 14 wamelipwa malimbikizo yao ya mishahara yenye thamani ya Tsh 668,089,055.
- ii) Jumla ya wafanyakazi 679 (Unguja 205 na Pemba 474) wameajiriwa. Aidha wafanyakazi 146 wamestaafu kazi kwa mujibu wa sharia, wafanyakazi 03 wamestaafu kwa hiari, wafanyakazi 04 wamechukua likizo bila ya malipo, mfanyakazi 01 amestaafu kwa ugonjwa, na wafanyakazi 24 wamefariki dunia, Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema peponi Amiin.
- iii) Vikao vya viongozi wakuu na wafanyakazi wote wa Wizara Unguja na Pemba wakiwemo maafisa elimu wa Mkoa na Wilaya, Waratibu wa Elimu, Waratibu wa vituo vya ubunifu na waratibu wa vituo vya walimu vimefanyika. Lengo la vikao hivyo ni kuimarisha utendaji na nidhamu kazini katika utoaji wa huduma bora na kwa wakati.
- iv) Jumla ya wafanyakazi 233 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu, wafanyakazi 72 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na wafanyakazi wapya 1,998 wamepatiwa mafunzo ya awali kazini.
- v) Jumla ya wafanyakazi 917 (596 Unguja na 321) Pemba wamepata mikopo ya fedha taslim, vifaa vya ujenzi, vipando na vifaa vya matumizi ya nyumbani katika

Taasisi mbali mbali za kifedha zikiwemo Benki na SACCOS.

Matokeo ya muda mfupi

Ufanisi katika utoaji wa huduma, Uongozi na Utawala umeimarika katika ngazi zote na hivyo kupelekea kuimarika katika utekelezaji wa malengo ya elimu.

Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti

45. Mheshimiwa Spika, Madhumuni makubwa ya Programu hii ni kufanikisha na kuratibu utekelezaji wa Mipango, Sera na Utafiti ya Wizara. Programu hii ndogo inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya **TSh. 10,999,859,000**. Kati ya fedha hizo, **TSh. 2,963,500,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, TSh. 824,319,000 ni kwa ya ajili ya malipo ya mishahara ya wafanyakazi na **TSh. 7,212,040,000** ni kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za Maendeleo. Hadi kufikia Aprili 2024 Jumla ya **TSh. 1,698,728,222** sawa na asilimia **15** zilipatikana. Utekelezaji halisi wa programu hii ni kama hivi ifuatavyo:-

- i. Rasimu ya Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya elimu wa miaka saba 2023- 2030 na mapitio ya Sera Mpya ya Elimu zimekamilika. Kufuatia mapendekezo ya ripoti ya mageuzi ya elimu, Wizara inaendelea na mapitio ya Sheria ya Elimu ili kuenda sambamba na mageuzi hayo na malengo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa. Aidha, Wizara imeunda kamati maalum ya usimamizi wa utekelezaji wa mpango wa mageuzi ya elimu.

- ii. Samani za wanafunzi, Komputa, vitanda, na samani kwa ajili ya walimu na maktaba zimenunuliwa kutoka China ambapo jumla ya makontena zaidi ya 88 kati ya 98 yenye samani hizo tayari yamewasili bandarini Zanzibar. Aidha, Makontena 30 kati ya hayo yameshatolewa na utaratibu wa kutoa kontena zaidi bandarini unaendelea.
- iii. Wizara imeanza utekelezaji wa miradi miwili mipya yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 61.7. Miradi hii ina lengo la kuimarisha ubora wa elimu ya lazima kwa kuwapatia walimu mafunzo, upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, matumizi ya TEHAMA katika elimu pamoja kuimarisha miundombinu ya skuli kwa kujenga skuli 7 mpya Unguja na Pemba. Aidha, utekelezaji wa mradi wa SEBEP wenye lengo la kuimarisha ujuzi wa vijana katika soko la uchumi wa buluu unaendelea, kwa sasa upo katika hatua za kuwapata washauri elekezi watakao sarifu michoro na kusimamia ujenzi wa miundombinu ya mradi ikiwemo ujenzi wa vyuo vitano vya Mafunzo ya Amali Unguja na Pemba na Chuo cha Ubaharia.
- iv. Wizara imekamilisha uhakiki wa data za utafiti wa SEACMEQ na kuwasilishwa katika nchi washiriki wa utafiti huo kwa uchambuzi zaidi kabla ya kuanza uandishi wa ripoti ya utafiti huo.
- v. Ujenzi wa jengo la ghorofa 4 (G+4) la Ofisi ya Wizara Pemba unaendelea na umefikia asilimia 30. Aidha, taratibu za manunuzi za kumpata mshauri elekezi

wa kuandaa michoro ya utanuzi wa jengo la Makao Makuu ya Wizara - Mazizini Unguja unaendeleo na mikataba inatarajiwa kutiwa saini mwanzoni mwa Mwezi wa Juni, 2024.

- vi. Ujenzi wa Ofisi Saba za Elimu za Wilaya umekamilika. Ofisi hizi pia zimejumuisha Maktaba, Ofisi ya Takwimu, TEHAMA na Ofisi za wakaguzi wa Elimu wa Wilaya. Aidha, Ofisi hizo zimepatiwa vifaa vya TEHAMA vikiwemo Kompyuta 10 kila moja, samani, printa, projector na mashine ya fotokopi. Ofisi nne kati ya hizo tayari zimeshafunguliwa na kuanza kutumika.
- vii. Wizara imeendelea kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa miradi ya elimu iliyokamilika na inayoendelea. Miongoni mwa miradi hiyo ni Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya lazima, Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi na Msingi na Mradi wa Uimarishaji wa Mafunzo ya Amali na Mradi wa uimarishaji wa Miundombinu ya Elimu.
- viii. Kitabu cha Takwimu za Elimu (Statistical Abstract 2019 -2023) kimekamilika na takwimu zimewasilishwa kwa wadau mbali. Aidha, Zoezi la Sensa ya Mwaka ya Skuli (Annual School Census) limekamilika.
- ix. Mkutano Mkuu wa Saba wa wadau wa elimu umefanyika kwa lengo la kutathmini maendeleo ya Sekta ya elimu kwa mwaka 2024 ukiwa umebeba kaulimbiu ya “Mabadiliko ya Elimu kwa Maendeleo Endelevu”. Jumla ya washiriki 150 walihudhuria

mkutano huo wakiwemo walimu, wajumbe wa kamati za skuli, Maafisa wa elimu kutoka Wilaya zote za Unguja na Pemba, wanasiasa, taasisi zisizo za kiserikali, Jumuiya za Kijamii, wahisani wa ndani na nje na viongozi mbalimbali kutoka sekta za Serikali.

Matokeo ya muda mfupi

- i) Utafiti mmoja umefanyika na ripoti inatarajiwa kuwasilishwa kwa wadau.
- ii) Rasimu ya Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya elimu wa miaka saba 2023-2030 imekamilika.
- iii) Ripoti za utekelezaji na tathmini ya maendeleo ya elimu imeandaliwa.
- iv) Mapendekezo ya miradi mipya miwili imeandaliwa na kuwasilishwa kwa washirika wa maendeleo.

Programu ndogo ya Uratibu shughuli za elimu Pemba

- 46. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ina madhumuni ya kuratibu na kusimamia shughuli zote za elimu kwa upande wa Pemba. Msimamizi Mkuu wa shughuli za programu hii ni Afisa Mdhamini wa Elimu Pemba. Programu hii ndogo ilipangiwa jumla ya **TSh. 3,766,154,277**. Kati ya fedha hizo, **TSh. 3,416,154,277** ni kwa ajili ya mishahara na **TSh. 350,000,000** ikiwa ni matumizi mengineyo. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya **TSh. 1,867,028,661** sawa na asilimia **50** zimepatikana. Fedha za programu hii zilitumika katika kusimamia na kufuatilia shughuli zote na programu za elimu Pemba.

MAPATO

47. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kukusanya mapato kupitia usajili wa Skuli za binafsi, malipo ya leseni za walimu, ada za usajili wa skuli, ada za kiingilio kwa wanafunzi wanaojiunga na kidato cha sita na usajili wa wanafunzi wa skuli binafsi wanaofanya mitihani ya Taifa na usajili wa vituo vya kufanyia mitihani. Hadi kufikia Aprili 2024, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imekusanya jumla ya **TSh. 263,884,529** kati ya **TSh. 396,396,336** zilizopangwa kukusanywa. Hii ni sawa ya asilimia 67 ya makadirio. Kati ya mapato yaliyokusanywa **TSh. 94,182,676.50** zinatokana na malipo ya leseni za walimu, **TSh. 38,614,932.50** za usajili wa skuli za binafsi, **TSh. 123,396,920** usajili wa wanafunzi wa skuli binafsi wanaofanya mitihani ya Taifa pamoja na usajili wa vituo vya kufanyia mitihani na **TSh. 7,690,000** za makusanyo ya ada za kiingilio kwa wanafunzi wanaojiunga na kidato cha sita.

MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2024/2025 KATIKA MFUMO WA PROGRAMU.

48. Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 naomba sasa niwasilishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa fedha 2024/2025 kwa kuzingatia vipaumbele vya Wizara.

Vipaumbele vya Wizara

49. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inaendelea kutekeleza

mapendekezo ya ripoti ya mageuzi ya sekta ya Elimu kwa kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

- i) Kuimarisha uongozi na usimamizi wa elimu katika ngazi zote za elimu zikiwemo Skuli, Wilaya, Mkoa na Wizara.
- ii) Kuimarisha mfumo wa tathmini ya maendeleo ya elimu ya wanafunzi katika ngazi zote za elimu na kupandisha ufaulu wao.
- iii) Kuimarisha miundonmbinu ya Elimu kwa kujenga madarasa 1500 kupitia ujenzi wa Skuli za Ghorofa, Skuli za Chini na kukamilisha madarasa yaliyoanzishwa na wananchi, kwa Unguja na Pemba, nyumba 20 za walimu, Ofisi ya Wizara, Ofisi 4 za Elimu Wilaya, vyoo 300, Dakhalia 8 zikiwemo dakhalia za wanaume za Chwaka Tumbe na Paje Mtule pamoja na kuzifanyia ukarabati mkubwa na mdogo skuli 100 za Msingi na Sekondari.
- iv) Kujenga karakana (workshop) za Elimu ya Amali katika skuli 33 za Sekondari Unguja na Pemba (karakana 3 kwa kila Wilaya) na kujenga uzio katika skuli ya Sekondari ya Hasnuu Makame na Mohamed Juma Pindua.
- v) Kuimarisha matumizi ya teknolojia katika kufundishia na kujifunzia kwa kuziunganisha na mkonga wa taifa taasisi za Elimu zikiwemo; skuli 217 za Sekondari, Vituo vya walimu 12 na Vituo vya Ubunifu wa Kisayansi (Hubs) 22 pamoja na kuzipatia vifaa vya TEHAMA.

- vi) Kuendelea kutekeleza mtaala mpya wa umahiri kwa elimu ya maandalizi, msingi na Sekondari kwa kuwapatia walimu mafunzo na vifaa vya kujifunzia na kufundishia vikiwemo vya Watoto wenye mahitaji maalumu.
- vii) Kuimarisha Mafunzo ya Ufundi na Amali kwa kujenga vyuo vitano vya Mafunzo ya Amali, utanuzi wa Chuo cha Karume (KIST) na ujenzi wa chuo cha ubaharia na kuzipatia vifaa.
- viii) Kuimarisha Elimu ya Juu kwa kuongeza fursa ya upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar kuanzia ngazi ya Diploma; kuanza mradi wa kujenga kampasi ya kudumu ya Chuo cha IIT Madrasa; Ujenzi wa Jengo la Skuli ya kilimo, Jengo la maabara ya sayansi ya kisasa- SUZA, Ujenzi wa skuli ya Afya, skuli ya meno na kliniki yake-SUZA.
- ix) Kuimarisha huduma za maktaba kwa kuanza kujenga maktaba mpya ya kisasa Pamoja na kuimarisha maktaba mtandao (e-library).

50. Mheshimiwa Spika, Sasa naomba kuwasilisha mpango wa maendeleo ya elimu kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa mfumo wa programu kama ifuatavyo:-

51. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali itaendelea kutekeleza malengo yake yaliyozingatia malengo ya Taifa ya Dira 2050, Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Malengo ya Maendeleo

Endelevu (SDG), Mapendekezo ya ripoti ya mageuzi ya Sekta ya Elimu Zanzibar, Ahadi za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na mikakati mengine ya kitaifa na kimataifa yenye lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma bora ya elimu nchini. Wizara pia, itaendelea kushirikiana na sekta nyengine zinazotoa huduma za jamii na kuimarisha uchumi ikiwemo Wizara ya Afya, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, Wizara ya Maji na Nishati, Idara maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha Wizara itaendeleza mashirikiano na washirika wa maendeleo wa ndani na nje na mashirika yasiyo ya kiserikali na wananchi kwa ujumla katika utekelezaji wa mpango wake kupitia programu sita na miradi mbalimbali ya maendeleo ya elimu.

52. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara itatekeleza miradi mitatu ya maendeleo ambayo ni:-

- i. Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya elimu
- ii. Mradi wa Uimarishaji wa Ubora wa Elimu kupitia Upatikanaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia, Mafunzo ya Walimu na Matumizi ya TEHAMA
- iii. Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Juu.

MAELEZO YA PROGRAMU ZA ELIMU

53. Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni maelezo ya programu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali yanayohusisha

Madhumuni, Matokeo ya muda mfupi, Viashiria na Shabaha za utekelezaji kwa kila programu.

PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI

54. Mheshimiwa Spika, Programu hii ina madhumuni ya kumuandaa mtoto kimwili na kiakili kwa ajili ya kupata elimu ya maandalizi na msingi na kumuwezesha kujua kusoma, kuandika na kuhesabu na kumtayarisha kwa elimu ya Sekondari. Jumla ya **TSh. 236,293,613,698** zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha kazi za programu hii. Kati ya fedha hizo, **TSh. 117,599,363,698** ni kwa kazi za kawaida na **TSh. 118,694,250,000** kwa kazi za maendeleo.

Matokeo ya muda mfupi

- Wanafunzi waweze kujua kusoma, kuandika na kuhesabu.

Viashiria vya matokeo

- Asilimia ya uandikishaji.
- Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi.
- Uwiano wa idadi ya walimu kwa wanafunzi.
- Uwiano wa wanafunzi kwa darasa.
- Asilimia ya Skuli zinazoendeshwa kwa mtindo wa shifti moja

Shabaha ya Utekelezaji

- Kuongeza kiwango cha uandikishaji wanafunzi wa maandalizi kutoka asilimia 84.3 kwa mwaka 2024 hadi kufikia asilimia 100 ifikapo mwaka 2025.

- Kuongeza kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa ngazi ya elimu ya msingi kutoka asilimia 104.4 kwa mwaka 2024 hadi kufikia asilimia 110 ifikapo mwaka 2025.
- Kupungua kwa uwiano wa idadi ya walimu kwa Wanafunzi ngazi ya maandalizi kutoka 29 mwaka 2024 hadi 27 mwaka 2025.
- Kupungua kwa uwiano wa idadi ya walimu kwa Wanafunzi ngazi ya msingi kutoka 42 mwaka 2024 hadi 45 mwaka 2025.
- Kupungua kwa Uwiano wa wanafunzi kwa darasa ngazi ya maandalizi kutoka 52 mwaka 2024 hadi kufikia 45 mwaka 2025.
- Kupungua Uwiano wa wanafunzi kwa darasa ngazi ya msingi kutoka 60 mwaka 2024 hadi kufikia 55 mwaka 2025.
- Kuongeza asilimia ya Skuli zinazoendeshwa kwa shifti moja kutoka asilimia 66.7 mwaka 2024 na kufikia asilimia 75 mwaka 2025
- Kuongeza asilimia ya ufaulu wa Wanafunzi katika mtihani wa Darasa la saba kutoka asilimia 95.3 ya mwaka 2023 hadi kufikia asilimia 96.1 mwaka 2024.

PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI

55. Mheshimiwa Spika, Programu ya Elimu ya Sekondari madhumuni yake makubwa ni kumtayarisha mwanafunzi aweze kuendelea na masomo katika ngazi za juu zaidi. Jumla ya **TSh. 242,537,540,535** zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha kazi za programu hii. Kati ya fedha hizo, **TSh. 111,428,040,535** ni kwa kazi za kawaida na **TSh. 131,109,500,000** kwa kazi za maendeleo.

Matokeo ya muda mfupi

- Kutoa Elimu ya Sekondari.

Viashiria vya matokeo

- Asilimia ya uandikishaji
- Asilimia ya wanafunzi wanaomaliza elimu ya lazima,
- Asilimia ya ufaulu wa wanafunzi na wanaoendelea katika ngazi ya kidato cha nne, cha sita na elimu ya juu.
- Uwiano wa idadi ya Wanafunzi kwa walimu.
- Uwiano wa wanafunzi kwa darasa.
- Asimilia ya Skuli zinazoendeshwa kwa mtindo wa shifti moja

Shabaha za utekelezaji

- Kuongezeka kiwango cha uandikishaji wanafunzi wa Sekondari ya awali (Kidato cha 1 – 4) kutoka asilimia

63.8 mwaka 2024 hadi kufikia asilimia 65.0 mwaka 2025.

- Kuongezeka kiwango cha ufaulu cha Wanafunzi wa kidato cha pili kutoka asilimia 91.2 mwaka 2023 hadi kufikia asilimia 92.3 mwaka 2024.
- Kiwango cha ufaulu cha Wanafunzi wa kidato cha nne kutoka asilimia 85.7 mwaka 2023 hadi kufikia asilimia 87.3 mwaka 2024.
- Kiwango cha ufaulu cha Wanafunzi wa kidato cha Sita kutoka asilimia 99.93 mwaka 2023 hadi kufikia asilimia 99.96 mwaka 2024.
- Kupungua kwa uwiano wa idadi ya walimu kwa Wanafunzi kutoka 20 Mwaka 2024 hadi 25 mwaka 2025.
- Kuongeza asilimia ya Skuli zinazoendeshwa kwa shifti moja kutoka asilimia 86 mwaka 2024 na kufikia asilimia 90 Mwaka 2025
- Kufikia Uwiano wa wanafunzi 45 kwa darasa mwaka 2025.

PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU

56 Mheshimiwa Spika, programu hii madhumuni yake ni kutoa elimu itakayomuwezesha muhitimu kujijiri au kuajiriwa. Jumla ya **TSh. 210,747,937,698** zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha kazi za programu hii. Kati ya fedha

hizo, **TSh. 35,981,775,698** ni kwa kazi za kawaida na **TSh. 174,766,162,000** kwa kazi za maendeleo. Programu hii ina programu ndogo moja na maeneo madogo manne ambayo ni:-

Programu ndogo ya Mafunzo ya Ualimu

- 57. Mheshimiwa Spika,** programu hii ina madhumuni ya kuwawezesha walimu kuwa wabunifu, wataalamu na wenye uwezo wa kuongoza ili kukuza ubora wa elimu.

Matokeo ya muda mfupi

- Uwepo wa walimu wenye umahiri watakaokuza ubora wa elimu itolewayo.

Viashiria vya matokeo

- Idadi ya Wanafunzi waliojiunga na vyuo vya ualimu.
- Idadi ya wanafunzi waliohitimu mafunzo ya ualimu.
- Idadi ya programu za mafunzo ya Ualimu
- Idadi ya walimu waliopatiwa mafunzo kazini
- Idadi ya walimu waajiriwa wapya waliopatiwa mafunzo.

Shabaha za Utekelezaji

- Kuongeza kiwango cha asilimia ya walimu wenye sifa kutoka 94 mwaka 2023 hadi kufikia asilimia 96 mwaka 2024.

- Kuongeza programu za mafunzo ya ualimu kutoka programu 1 ya mafunzo tarajali (pre – service training) mwaka 2024 hadi kufikia programu 8 Mwaka 2025
- Kuongeza idadi ya Wanafunzi waliohitimu mafunzo ya Ualimu kutoka 836 mwaka 2023 hadi kufikia 1,669 mwaka 2024.
- Kuongeza idadi ya Walimu waliopatiwa mafunzo kazini kutoka 2,778 mwaka 2024 hadi kufikia 3,200 mwaka 2025.
- Kuongeza idadi ya Walimu waajiriwa wapya waliopatiwa mafunzo kutoka 252 mwaka 2023 hadi kufikia 1,600 mwaka 2025.

Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti

58. Mheshimiwa Spika, Huduma hii ina madhumuni ya kumtayarisha mwanafunzi kuingia katika fani za kitaalamu na ajira.

Matokeo ya muda mfupi

- Ongezeko la wahitimu wa kiwango cha elimu ya Stashahada, Shahada ya kwanza, Shahada ya pili na Shahada ya tatu katika fani mbali mbali za kitaalamu zinazohitajika katika maendeleo ya nchi.

Viashiria vya matokeo

- Kuanzisha kigoda cha kitaaluma cha kuenzi mchango wa Sheikh Abeid Amani Karume Rais wa kwanza wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

- Idadi ya wanafunzi wanaomaliza ngazi ya Astashahada na Stashahada.
- Idadi ya wanafunzi wanaomaliza ngazi ya Shahada ya kwanza ya Uzamili na Uzamivu.
- Idadi ya Programu mpya zinazoanzishwa
- Idadi ya tafiti na ushauri elekezi zilizofanywa.

Shabaha za Utekelezaji

- Uwepo wa kigoda cha kitaaluma cha kuenzi mchango wa Sheikh Abeid Amani Karume Rais wa kwanza wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Kufundisha na kuongeza idadi ya Wanafunzi wanaomaliza ngazi ya mbalimbali za shahada na stashahada kutoka 2,102 mwaka 2024 hadi kufikia 2,400 mwaka 2024.
- Kuongeza programu mpya za masomo kutoka programu mbili mpya zilizoanzishwa mwaka 2023 na kufikia programu 4 mwaka 2024.
- Kuongezeka kwa huduma za ushauri elekezi na tafiti kwa wahadhiri wa Chuo.

Huduma ya Elimu ya Sayansi na Teknolojia

59. Mheshimiwa Spika, Huduma hii ina madhumuni ya kuimarisha elimu ya sayansi na teknolojia.

Matokeo ya muda mfupi

- Kuongeza wahitimu wa fani za Ufundi, Uhandisi, Sayansi, na Teknolojia.

Viashiria vya matokeo

- Idadi ya Wanafunzi wa fani za Ufundi, Uhandisi, Sayansi, na Teknolojia walioandikishwa
- Idadi ya wahitimu wa fani za Ufundi, Uhandisi, Sayansi, na Teknolojia.

Shabaha za Utekelezaji

- Ongezeko la Idadi ya wanafunzi wa fani za Ufundi, Uhandisi, Sayansi, na Teknolojia walioandikishwa kutoka 522 Mwaka 2023/2024 na kufikia 623 mwaka 2024/2025.
- Ongezeko la Idadi ya wahitimu wa fani za Ufundi, Uhandisi, Sayansi, na Teknolojia kutoka 2,524 mwaka 2023/2024 na kufikia 2,619 mwaka 2024/2025.

Huduma ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu

60. Mheshimiwa Spika, Huduma hii ina madhumuni ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya Juu.

Matokeo ya muda mfupi

- Ongezeko la wanafunzi walionufaika na mikopo ya elimu ya juu.
- Ongezeko la wanafunzi wanaorejesha na mikopo ya elimu ya juu.

- Ongezeko la fedha zilizorejeshwa kutoka kwa wanafunzi walionufaika na mkopo.
- Ongezeko la Wanafunzi waliopatiwa ufadhili wa masomo

Viashiria vya matokeo

- Idadi ya wanafunzi waliopatiwa mikopo
- Idadi ya wanafunzi waliorudisha mikopo.
- Jumla ya fedha za marejesho ya mkopo zilorejeshwa.
- Idadi ya Wanafunzi waliopatiwa ufadhili wa SMZ
- Idadi ya Wanafunzi waliopatiwa ufadhili wa masomo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo

Shabaha za Utekelezaji

- Kuongeza utoaji wa mikopo kwa wanafunzi kutoka wanafunzi 6,060 ya waombaji mwaka 2023/24 hadi kufikia wanafunzi 7,367 ifikapo mwaka 2024/25.
- Kuongeza makusanyo ya marejesho ya mikopo kutoka TSh. 4.44 bilioni ya mwaka 2023/24 na kufikia TSh.5. 5 billioni mwaka 2024/25.
- Kuongeza Idadi ya Wanafunzi waliopatiwa ufadhili wa SMZ kutoka Wanafunzi 17 kwa mwaka 2023/24 hadi kufikia Wanafunzi 47 kwa mwaka 2024/25.
- Kuongeza Idadi Wanafunzi waliopatiwa ufadhili wa masomo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kutoka

Wanafunzi 59 kwa mwaka 2023/2024 hadi kufikia
Wanafunzi 65 kwa mwaka 2024/25.

Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu

61. Mheshimiwa Spika, Huduma hii ina madhumuni ya usimamizi na tathmini ya elimu ya juu.

Matokeo ya muda mfupi

- Kuimarika kwa mahusiano na mashirikiano mazuri ya uendeshaji wa taasisi za elimu ya juu.
- Ongezeko la wanafunzi wanaopata udhamini wa kujiunga na vyuo vya elimu ya juu.

Viashiria vya matokeo

- Idadi ya wanafunzi wanaojiunga na vyuo vya elimu ya juu ndani na nje ya nchi
- Idadi ya wanafunzi wanaopata udhamini wa kujiunga na vyuo vya elimu ya juu.

Shabaha za Utekelezaji

- Kuongeza idadi ya wanafunzi wa Vyuo vikuu kutoka 12,169 mwaka 2023 hadi 12,225 kufikia mwaka 2024.
- Kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaopata udhamini wa kujiunga na vyuo vya elimu ya juu.

PROGRAMU YA NNE: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI

62. Mheshimiwa Spika, Programu hii madhumuni yake ni kutoa elimu ya mafunzo ya amali kwa mwanafuzi kulingana na mahitaji ya soko la ajira. Jumla ya **TSh. 41,002,809,755** zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha kazi za programu hii. Kati ya fedha hizo, **TSh. 11,502,809,755** ni kwa kazi za kawaida na **TSh. 29,500,000,000** kwa kazi za maendeleo. Programu hii ina programu ndogo mbili kama ifuatavyo:-

Programu ndogo ya Mafunzo ya Amali

63. Mheshimiwa Spika, Programu hii ina madhumuni ya kutoa elimu itakayowawezesha vijana kujijari ili kujikwamua na umasikini.

Matokeo ya muda mfupi

- Ongezeko la wahitimu waliopata Mafunzo ya Amali na ufundi na kuweza kujijari.

Viashiria vya matokeo

- Idadi ya wanafunzi waliojiunga na Mafunzo ya Amali
- Idadi ya vikundi vya wahitimu wa Mafunzo ya Amali waliopata Mkopo na kujiari.
- Idadi ya wahitimu wa Mafunzo ya Amali

Shabaha za Utekelezaji

- Kuongezeka kwa vijana waliojiari kutoka vikundi 28 mwaka 2024 hadi kufikia vikundi 36 mwaka 2025.

- Kuongezeka idadi ya wanafunzi wanaoijiunga na mafunzo ya amali kutoka wanafunzi 2,217 kwa mwaka 2024 hadi kufikia wanafunzi 2,439 kwa mwaka 2025.
- Kuongezeka idadi ya wahitimu wa mafunzo ya amali kuongezeka kutoka wahitimu 860 mwaka 2023 hadi kufikia wahitimu 1,166 kwa mwaka 2024.

Programu ndogo ya Elimu Mbadala na Watu Wazima

64. Mheshimiwa Spika, Programu hii ina madhumuni ya kupunguza kiwango cha kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu miongoni mwa wanajamii.

Matokeo ya muda mfupi

- Ongezeko la vijana waliorejea masomo baada ya kuacha skuli
- Ongezeko la watu walioijiunga na madarasa ya wanakisomo

Viashiria vya matokeo

- Idadi ya wanafunzi waliorejeshwa skuli
- Idadi ya vijana wanaoijiunga na madarasa ya elimu mbadala
- Idadi ya watu wazima wanaoijiunga katika madarasa ya wanakisomo,
- Idadi ya vijana walioijiunga vituo vya elimu kujiendeleza

Shabaha za Utekelezaji

- Kuongeza idadi ya Vijana wenye umri kati ya miaka 7 hadi 14 waliorejeshwa skuli imeongezeka kutoka vijana 31,639 mwaka 2023/2024 hadi kufika vijana 35,000 mwaka 2024/2025.
- Kuongeza idadi ya wanaojiunga katika madarasa ya wanakisomo.
- Kuandikisha vijana 1,200 wenye umri kati ya miaka 15 hadi 22 waliokosa fursa ya masomo katika Vituo vya Elimu Mbadala.

PROGRAMU YA TANO: UBORA WA ELIMU

Mheshimiwa Spika, Programu hii ina madhumuni ya kutoa elimu bora kwa ngazi zote za elimu. Jumla ya **TSh. 48,565,662,396** zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha kazi za programu hii. Kati ya fedha hizo, **TSh. 14,920,662,396** ni kwa kazi za kawaida na **TSh. 33,645,000,000** kwa kazi za maendeleo. Programu hii ina programu ndogo tatu na maeneo matano ya kutoa huduma kama yafuatayo:-

Huduma ya Mitaala na Vifaa vya Kufundishia

65. Mheshimiwa Spika, Huduma hii ina madhumuni ya kutayarisha mitaala ya elimu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ngazi za elimu ya maandalizi, msingi, Sekondari na mafunzo ya Ualimu.

Matokeo ya muda mfupi

- Uwepo wa Mitaala ya Elimu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ngazi zote za elimu.

Viashiria vya matokeo

- Idadi ya Mitaala iliyotayarishwa
- Idadi ya vitabu vilivyochapishwa na kusambazwa katika skuli.
- Idadi ya walimu waliopatiwa mafunzo ya mtaala mpya wa umahiri.

Shabaha za Utekelezaji

- Kuandaa Mtaala wa Mafunzo ya Ualimu
- Kuchapisha vitabu vya masomo ya mtaala mpya na kuvisambaza katika skuli
- Kutoa mafunzo kwa walimu kuhusu mtaala mpya

Huduma ya Upimaji na Tathmini ya Elimu

66. Mheshimiwa Spika, Programu hii ina madhumuni ya kupima na kutathmini utekelezaji wa utoaji wa elimu.

Matokeo ya muda mfupi

- Upimaji wa wanafunzi katika mitihani yao ya taifa.

Viashiria vya matokeo

- Asilimia ya ufaulu kwa mada katika mitihani ya taifa

Shabaha ya Utekelezaji

- Kuandaa na kuwapima wanafunzi kwa mitihani na kutoa ripoti ya ufaulu wa wanafunzi kwa kila mada kwa mujibu wa mitaala.

Huduma ya Ukaguzi wa Elimu

67. Mheshimiwa Spika, utoaji wa huduma hii una madhumuni ya kusimamia utoaji wa elimu unaofuata mtaala na kuhakikisha ufanisi na ubora wa elimu inayotolewa.

Matokeo ya muda mfupi

- Ongezeko la Skuli na walimu waliofanyiwa ukaguzi

Viashiria vya matokeo

- Idadi ya skuli na walimu ziliofanyiwa ukaguzi

Shabaha za Utekelezaji

- Kuongeza idadi ya skuli zilizokaguliwa kutoka skuli 980 mwaka 2023/2024 na kufikia skuli 1,024 (687 Unguja na 337 Pemba) kwa mwaka 2024/2025.
- Kuongeza idadi ya walimu waliokaguliwa kutoka 2,800 kwa mwaka 2023/2024 hadi kufikia 2,900 kwa mwaka 2024/2025

Huduma za Maktaba

68. Mheshimiwa Spika, Programu hii ina madhumuni ya kutoa fursa ya kutumia vitabu na vyanzo vyengine vya taaluma kwa wananchi.

Matokeo ya muda mfupi

- Ongezeko la wanafunzi, vijana na wanajamii wanaopatiwa huduma za maktaba.
- Ongezeako la vituo vya huduma za maktaba ili kufikisha huduma kwa jamii.
- Ongezeko la vitabu na vifaa vya kusomea katika maktaba.
- Uwepo wa maktaba mtandao (E-library.)

Viashiria vya matokeo

- Idadi ya watu wanaotumia maktaba
- Idadi ya vitabu, CDs, vifaa vya elektroniki, magazeti na majarida yaliyopo katika maktaba.
- Idadi ya skuli zenye maktaba kamili.
- Idadi ya maktaba za zilizozoanzishwa
- Uwepo wa jengo jipya la kisasa la maktaba

Shabaha za Utekelezaji

- Kuongeza idadi ya wanachama waliosajiliwa kutoka 562 mwaka 2024 hadi kufikia wanachama 682 mwaka 2025.
- Kuongezeka kwa idadi ya watumiaji wa maktaba kutoka 44,942 mwaka 2024 hadi kufikia watumiaji 55,000 mwaka 2025.

- Kuongeza idadi ya maktaba za Wilaya kutoka maktaba saba mwaka 2024 hadi kufukia maktaba 11 mwaka 2025.
- Kujenga maktaba kuu ya Taifa

Huduma ya Urajisi wa Elimu

69. Mheshimiwa Spika, Programu hii ina madhumuni ya kuhakikisha Sheria, Sera na taratibu za Wizara zinafuatwa, kutoa leseni kwa walimu na kusajili skuli za Serikali na za binafsi.

Matokeo ya muda mfupi

- Skuli za Serikali na binafsi zenye viwango bora kusajiliwa
- Leseni za walimu kutolewa.
- Kuondoa matukio ya udhalilishaji kwa wanafunzi

Viashiria vya matokeo

- Idadi ya leseni za walimu zilizotolewa.
- Idadi ya skuli zilizosajiliwa.
- Idadi ya kesi za ndoa kwa wanafunzi zilizofuatiliwa na kutolewa uamuzi.

Shabaha za Utekelezaji

- Kuongeza idadi ya leseni za walimu kutoka leseni 3,240 kwa mwaka 2023/2024 hadi kufikia leseni 7,000 kwa mwaka 2024/2025.

